Nipashe

Jumamosi Agosti 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya

ISSN 0856 • Na. 0581414

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

tigo pesa SportPesa MAOKOTO Deilee! WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Watanzania 200 wapatiwa huduma upandikizaji mimba**

UKURASA 2




UKURASA 11

# Mambo mazito saba kwa Malasusa KKKT

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### WAZIRI AVUNJA UKIMYA KUHUSU NDEGE YA RAIS

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amevunja ukimya kuhusu ndege ya Rais huku akiwataka wananchi....

UKURASA WA 4

### JK AONGOZA MAMIA MAZISHI YA PROF. MAHALU

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, jana aliongoza mamia ya wananchi kuaga mwili wa mwasisi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Willium Mahalu, ambaye...

UKURASA WA 5

### MACHINGA WAKUBALI KULIPA KODI 100,000/-


WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu kama machinga, wamekubali kulipa kodi ya Sh. 100,000 kwa mwaka kila mmoja, kiwango ambacho...

## Wazazi walia mtuhumiwa wa ubakaji kutofikishwa kortini

UKURASA 2

**ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, juzi alichaguliwa kuwa Mkuu wa Kanisa hilo nchini. Kutokana na kuchaguliwa huko, watu wa makundi mbalimbali wameainisha mambo saba ambayo wanabainisha ni changamoto katika uongozi wake...**

*Endelea Ukurasa 3*



Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Alex Malasusa

MICHEZO GAMONDI ATAKA MABAO, SOKA SAFI LEO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

## Waziri avunja ukimya kuhusu ndege ya Rais

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amevunja ukimya kuhusu ndege ya Rais huku akiwataka wananchi kupuuza taarifa za uzushi zinazosambazwa na watu wasio wema kwamba inashikiliwa Dubai.

Simbachawene aliyasema hayo jana wakati akizindua Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali katika Kituo cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

"Mtu anaweza kuzusha jambo na likawapotezea muda mwingi wananchi badala ya kufanya mambo ya maendeleo, kwa mfano uzushi kuhusiana na ndege ya Rais Gulf Stream (G550) kuzuiwa Dubai.

"Nataka niwahakikishie Watanzania kuwa ndege hiyo iko sehemu husika kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Terminal One VIP, jijini Dar es Salaam kwenye eneo ambalo Wakala wa Ndege za Serikali wanalitumia na yeyote anayepita barabarani ataiona," alisema.

Simbachawene alisema akiwa waziri mwenye dhamana ya utawala bora ameona aliweke wazi jambo hilo, lililoleta taharuki ili kuwaondoa hofu Watanzania na uvumi huo.

"jambo hili lisiwapotezee muda. Wanaovumisha hayo kwa nia ovu wanaweza kwenda kupata uhakika uwapo wa ndege hiyo. Viongozi wanasafiri kama kawaida kwa kutumia ndege hiyo," alisisitiza.

Simbachawene alitoa wito kwa Wajumbe wa bodi hiyo kushirikiana na menejimenti ya TGFA ili kuiwezesha wakala hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

"Ni matarajio yangu kuwa bodi hii itasimamia vema utendaji wa wakala ili kuleta tija kwa maendeleo ya taifa kama inavyosisitizwa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali, Prof. Idrissa Mshoro, alimwahidi Waziri Simbachawene kuwa yeye na wajumbe wa bodi hiyo kwa kushirikiana na menejimenti ya TGFA watatekeleza yote ambayo ameyaelekeza.

Alisema wanafahamu kwa kina maono makubwa ya Rais, Samia katika kuharakisha maendeleo ya nchi katika kuhakikisha uwapo wa usafiri madhubuti.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TGFA, Kapteni Budodi Budodi alisema menejimenti ya wakala inamhakikishia Waziri Simbachawene kuwa itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu pamoja na maelekezo ya bodi ili kufikia malengo ya uanzishwaji wa wakala.

# Wazazi walia mtuhumiwa wa ubakaji kutofikishwa kortini

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZAZI wa wanafunzi wawili wa Shule ya Msingi Kambarage, Kibaha mkoani Pwani, wamemlalamikia mtu anayedaiwa kuhusika na vitendo vya ubakaji kwa watoto wao kutofikishwa mahakamani ikiwa ni miezi sita tangu watoe taarifa polisi.

Watoto hao walibainika kufanyiwa vitendo hivyo Februari, mwaka huu, baada ya kupimwa na kumtaja mtuhumiwa kuwa ni Collin Jackson ambaye alikamatwa na kufikishwa polisi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Hassan Kikoko, mkazi wa Mwanalugali, ambaye ni mmoja wa wazazi wa watoto hao, alisema mpaka sasa imepita miezi sita bila mtuhumiwa huyo kufikishwa mahakamani pamoja na ushahidi uliowasilishwa na watoto hao.

Kikoko alisema baada ya watoto wao kumweleza mwalimu wakiwa shuleni, wazazi waliitwa na kushiriki katika hatua zote za kufikisha suala hilo polisi na kupimwa hospitalini.

"Februari 13, mwaka huu, watoto walianza kupimwa katika Kituo cha Afya cha Mkoani. Miezi mitatu baadaye, tuliitwa tena polisi tukaambiwa twende Hospitali ya (Teule yua Rufani ya Mkoa) Tumbi, Kibaha kwa ajili ya vipimo zaidi na hii ilikuwa awamu ya tatu watoto wanapimwa.

"Baada ya hapo watoto wakahojiwa kwa mara nyingine katika Kituo cha Polisi Mji Mdogo Kibaha, Mei 13, mwaka huu, na tukapewa taarifa ya kusubiri wito kwa ajili ya mtuhumiwa kufikishwa mahakamani," alisema.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, tangu Mei hadi sasa, hakuna taarifa waliyopata kuhusiana na hatua zaidi na mwezi huu walilazimika kurudi polisi kufuatilia na kuelezwa kwamba jalada liko kwa Mwendesha Mashtaka.

Kikoko na mwenzake walisema walipofika Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkoa wa Pwani, walielekezwa kuandika barua kuelezea hatua zote tangu awali na Agost 22, mwaka huu, waliiwasilisha kusubiri hatua zaidi.

Mzazi huyo alibainisha kwamba mtuhumiwa ni jirani yake na kwamba alikuwa akikutana na watoto hao wenye umri wa miaka minane na mwingine tisa nyumbani anakoishi na kuwafanyia kitendo hicho kwa zamu na kwamba alianza kufanya hivyo tangu mwaka 2021 kwa nyakati tofauti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi (ACP) Pius Lutumo, alipoulizwa kuhusiana na suala hilo, alisema watoto hao tayari wamefanyiwa vipimo na mtuhumiwa alikamatwa na kuachiwa kwa dhamana.

Lutumo alisema upelelezi kuhusiana na tuhuma hizo unaendelea ikiwamo kupata ushahidi ili hatua ya mahakamani ifuate.

Mmoja wa walimu kwenye moja ya shule Mjini Kibaha (jina linahifadhiwa) alieleza hali ya wazazi kupunguza malezi na kujikita kwenye shughuli zao, huchangia kasi ya mabadiliko ya watoto kitabia na kuwapo kwa vitendo vya ubakaji.

Mwalimu huyo alisema hali bado ni mbaya kwenye shule kuhusiana na vitendo vya ukatili kwa watoto wa kike na wa kiume jambo ambalo linahitaji elimu kwa wazazi na jamii nzima.

Alisema kitendo cha baadhi ya watoto kuanza kuelezea matukio ya kikatili kimetokana na elimu inayotolewa ya kuwapa ujasiri wa kueleza wanayofanyiwa kinyume na haki zao.



Mratibu wa mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP), Mhandisi John Skauki (wa pili kushoto), akifafanua jambo kwa baadhi ya wajumbe wa menejimenti ya Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Aboubakar Issa (kulia) na Mhandisi Decklan Mhaiki (kushoto) walipotembelea mradi huo, wilayani Rufiji mkoani Pwani, jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watanzania 200 wapatiwa huduma ya upandikizaji ujauzito nchini India

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha Chennai Fertility (CFC) cha India kimesema Watanzania 200 wamepatiwa huduma ya upandikizaji mimba (IVF) nchini humo, baada ya kushindwa kupata ujauzito kibaolojia.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa CFC Bingwa wa Uzazi na Watoto wa Kupandikiza, Dk. Vadingadu Thomas, alisema kituo hicho kimefanikisha huduma hiyo kwa idadi ya watanzania hao.

Katika Maonyesho ya Kimataifa ya Bidhaa za Dawa na Vifaa Tiba 2023 yanayofanyika Dar es Salaam, bingwa huyo alisema tangu kuanza kutolewa huduma hiyo nchini India kwa zaidi ya miaka 20, takribani watoto 65,000 wamezaliwa kupitia IVF.

"Tunatarajia kuanzisha huduma hii Tanzania hapa Dar es Salaam kwa watu wanaohitaji na hawana nauli ya kwenda India. Miezi sita ijayo tutafungua tawi la Chennai ili kuongeza huduma ya IVF," alisema.

Mwakilishi wa Chennai nchini, Doreen Luoga, alisema huduma inayotolewa na kituo hicho matokeo ni asilimia 80 hadi 90 na kuwataka Watanzania kutumia fursa ya kufika kwenye maonyesho hayo kupatiwa huduma bure kwa ajili ya matibabu zaidi.

"Kwenye maonyesho haya huduma za kibingwa zinatolewa bure kutoka kwa Daktari Bingwa, Thomas, hii ni fursa kwa watanzania wenye matatizo ya uzazi na mengine. Tunatoa huduma hapa kuanzia asubuhi hadi jioni. Ukihudumiwa na Chennai uhakika wa mama kupata ujauzito ni wa kiwango kikubwa kutokana na mabingwa waliopo na utaalamu walio nao, hata kwa walio zaidi ya miaka 50 hufanikiwa," alisema.

Luoga alibainisha kwamba wanaopatiwa huduma hiyo huwa chini ya uangalizi wa siku zisizopungua 90, ili mwanamke kufanikisha ujauzito kupitia mfumo huo wa kiteknolojia.

# Mambo saba mazito kwa Malasusa KKKT

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

HATIMAYE Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limempata Mkuu Mpya wa kurithi Askofu Frederick Shoo ambaye amemaliza muda wa kuliongoza baada ya kutumika kwa vipindi viwili mfululizo.

Huyo si mwingine bali ni Askofu Dk. Alex Malasusa wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Anarejea tena kwenye nafasi hiyo aliyoihudumu kuanzia mwaka 2007 hadi 2015 na kumpisha Askofu Dk. Shoo.

Askofu Dk.Malasusa alichaguliwa juzi usiku na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 21 wa KKKT, ulioanza Agosti 20 hadi 25 katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kilichoko Usa River, Arusha, baada ya mchuano mkali uliompa ushindi katika duru ya tatu.

Katika matokeo ya uchaguzi huo yaliyotangazwa na Mwenyekiti wa uchaguzi, Askofu Amon Mwenda wa Dayosisi ya Ruvuma, Dk. Malasusa alichaguliwa kwa kishindo kwa kura 167 sawa na asilimia 69.3, huku mpinzani wake, Askofu Dk. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi akipata kura 73, sawa na asilimia 30.7.

**MAMBO MAZITO**

Kutokana na kuchaguliwa kuliongoza kanisa hilo, baadhi ya watu wameeleza mambo saba ambayo yanaonekana kuwa changamoto katika utumishi wa nafasi hiyo.

Jambo la kwanza, ni kwamba anaingia katika uongozi huku KKKT ikiwa na katiba moja tofauti na mwanzo ambapo kila dayosisi ilikuwa na katiba yake na kufanya mambo yake ya ndani bila kuingiliwa na makao makuu ya kanisa. Katiba hiyo mpya ya KKKT ilipitishwa juzi na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 21 wa Kanisa kwa asilimia 86 ambazo ni zaidi ya theluthi mbili zinazotakiwa kikanuni.

Kabla ya kuwa na katiba moja, ilikuwa vigumu makao makuu kuingilia baadhi ya mambo ya ndani ya dayosisi jambo ambalo hata baadhi ya timu zilizoundwa kuchunguza tuhuma katika baadhi ya dayosisi, zilishindwa au kupata upinzani.

Timu hizo wakati mwingine zilikosa ushirikiano na hata kuchochea migogoro na migawanyiko katika dayosisi husika kama ilivyokuwa mgogoro wa Dayosisi ya Konde. Pia baadhi ya maaskofu walikuwa wakituhumiwa kutishia kujitenga na kuanzisha taasisi mpya isiyofungamana na KKKT.

Kutokana na mabadiliko hayo, katiba mpya inampa nguvu ya kusimamia Dayosisi zote 27, jambo ambalo ni changamoto kwa kuwa linaanza kutekelezwa sasa.

**TOFAUTI ZA MAASKOFU**

"Mtuombee sana kwani Nyumba ya Maaskofu haina umoja, kuna tofauti na mgawanyiko mkubwa," alisema Askofu mmoja (jina linahifadhiwa) kutokana na tofauti zilizotokana na mgawanyiko wa waziwazi baina ya maaskofu mwaka 2019 wakati Askofu Dk. Shoo alipopendekezwa kugombea nafasi ya Mkuu wa Kanisa kwa mara ya pili.

Katika mkutano huo, baadhi ya maaskofu walikuwa wakirushiana maneno kuonyesha kuwa hawaafikiani katika masuala mbalimbali ndiyo maana uchaguzi huo ulikuwa na upinzani.

Kutokana na mgawanyiko na tofauti za kimtazamo miongoni mwa maaskofu. Dk. Malasusa anakabiliwa na kibarua kizito cha kutatua tofauti hizo.

**UHUSIANO NA SERIKALI**

Mtihani mwingine alionao ni kujenga uhusiano mpya kati ya kanisa na serikali. Ana kazi ya kulitengeneza hilo kwa kuwa imekuwa inaonekana kwa nyakati fulani kuna misuguano baina ya pande hizo.

Katika baadhi ya mambo, baadhi ya viongozi wa kanisa wakiwamo maaskofu wamekuwa wakitoa kauli ambazo zilionekana dhahiri kuwa zinakinzana na misimamo ya serikali.

**UMOJA KKKT**

Kuwapo kwa utaratibu katika kila dayosisi kulionyesha kuwapo kwa umoja usio wa dhati bali ulionekana wakati wa matukio kadhaa hasa wakati wa kuingizwa kazini au msiba wa kiongozi wa dayosisi. Kunapotokea tukio kama hilo, maaskofu na maofisa waandamizi wengi kutoka takriban dayosisi zote wamekuwa wakikutana.

Wakati hayo yamekuwa yakifanyika, kila dayosisi imekuwa ikimiliki mali zake na kufanya mambo kipekee. Mfano ni suala la elimu, baadhi ya dayosisi zinamiliki vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na shule za sekondari ambazo hazina uhusiano wowote na KKKT.

Mfano, miaka ya 1990 KKKT ilianzisha Chuo Kikuu cha Tumaini ambacho kilikuwa na vyuo vikuu vishiriki kadhaa lakini baada ya muda, baadhi ya dayosisi zilijitoa na kumiliki vyuo vikuu ambavyo kanisa halina sauti navyo.

**SAKATA LA MUFINDI**

Jambo lingine ambalo ni changamoto kwa kiongozi huyo ni suala la Mufindi kuwa na uhuru wake kwa maana ya kuwa dayosisi. Jimbo la Mufindi lilitangaza kujitenga kutoka Dayosisi ya Kusini (Njombe) Mei, 2016 baada ya waumini wake kutangaza kuhama na kujiunga na Dayosisi ya Iringa.

Kutokana na mgogoro huo, Mkuu wa KKKT anayemaliza muda wake, Askofu Dk. Shoo, aliunda tume maalumu kwa ajili ya kutafuta suluhisho la kudumu jambo ambalo linapaswa katika uongozi wake kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu na hatimaye kuwa historia.

**SUALA LA KARATU**

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu wa Karatu kuwa wameshindwa kupewa uhuru wa kujiendesha. Hata baadhi wamekuwa wakidai kuwa wanakaliwa kimabavu na Dayosisi ya Kaskazini kwa kufanywa kama jimbo wakati kuna uwezekano wa kuwa dayosisi. Hili ni suala ambalo Dk. Malasusa anapaswa kulishughulikia akiwa mkuu mpya wa kanisa.

**DAYOSISI YA KONDE**

Licha ya kwamba mgogoro wa Dayosisi ya Konde ulimalizika baada ya kuwapo mabadiliko ya uongozi bado kuna dalili za kuwapo mgawanyiko miongoni mwa waumini, wakuu wa majimbo na wachungaji na waumini.

Kwa mantiki hiyo, Askofu Dk. Malasusa, ambaye kiasili anatoka Mbeya, ana kibarua kuhakikisha hali inatengemaa na umoja ndani ya dayosisi hiyo unarejea kwa ustawi wa kanisa.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED na MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) au Siku Saba (7) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ABUU IDDY RAMADHANI | IBRAHIM M MRISHO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | KILIMA HEWA JUU, WAZO, MANISPAA YA KINONDONI | 16/09/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 2 | DEVIS AGENCY (T) LIMITED | OCTAVIAN JOHN CHUWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na.DSMT1002617 | KIBAMBA, MANISPAA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 12/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 3 | LOLY COLLECTION LTD | DANIEL AUGUSTINO | SHAMBA Na.1310, LENYE HATI MILIKI No.38729 | BOKO, DOVYA, MANISPAA YA KINONDONI | 09/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 4 | MUSA IDDI MAKENYA | MUSA IDDI MAKENYA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MWEMBE BAMIA, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 02/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (*Marudio ya Mnada*) | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 5 | PATRICIA ANURUPHAS MPANJU | ANURUPHAS MPANJU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | NYAKASANGWE ,WAZO MANISPA YA KINONDONI | 09/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 6 | ALLY RAJABU KITIMU | ALLY RAJABU KITIMU & LATIFA ADELY SHIYO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI No.173724 | KILUNGULE- A, KIMARA, MANISPA YA UBUNGO | 12/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 7 | MOHAMED ABDALAH MWINYIKONDO | ZAINA ALLY MSOLIMA | NYUMBA YENYELESENI YA MAKAZI No.KND008502 | KINONDONI SHAMBA, MANISPAA YA KINONDONI | 14/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 8 | MOHAMED ABDALAH MWINYIKONDO | MOHAMED ABDALAH MWINYIKONDO | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MINONDO ,GEZAULOLE MANISPAA YA KIGAMBONI | 16/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 9 | ANDRONIUS ROMWALD KALISA | ANDRONIUS ROMWALD KALISA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANI SERIKALI MTAA | MALAMBA MAWILI, MBEZI MANISPAA YA UBUNGO | 18/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 10 | ANDRONIUS ROMWALD KALISA | ROMUADI A. KALISA | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | KEREGE , BAGAMOYO MKOA WA PWANI | 20/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**
**P.O. Box 1305**
**Songea, Ruvuma**
**Tel: 0716070298/ 0754881926/ 0784718734**
**Email: twinscoltd5@gmail.com**

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**
**P.O.Box 12943**
**Arusha**
**Tel: 0752 632 033/ 0628512033**
**Email: mangwembe@gmail.com**



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja mahusiano na uwajibikaji wa kampuni ya madini ya Kudu Graphite, Vickey Puncheon (kushoto), wakati akikagua mabanda ya maonyesho ya madini na uwekezaji, wilayani Ruangwa mkoani Lindi jana. Wengine ni wataalamu wa Giologia wa kampuni hiyo, Peter Malley na Benjamini Kisawike. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JK aongoza mamia mazishi Prof. Mahalu

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, jana aliongoza mamia ya waombolezaji kumuaga aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. William Mahalu, ambaye alizikwa jana katika makaburi ya Kinondoni.

Prof. Mahalu ambaye aliyefariki dunia Agosti 20, mwaka huu, akipatiwa matibabu JKCI, ibada ya kumuaga ilifanyika Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT), Magomeni, Dar es Salaam na kuongozwa na Askofu wa Dayosisi ya Pwani ya kanisa hilo, Philipo Mafuja.

Ibada hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, na wanataaluma sekta ya afya.

Akiongoza ibada hiyo, Askofu Mafuja alisema wanadamu wanapaswa kuishi maisha yenye kusudi la Mungu kwa kuwa kila mmoja ameletwa duniani kwa kusudio maalumu, hivyo ili kuacha alama, kuna umuhimu wa kuitumikia jamii.

"Binadamu tunaishi kwa kusudio lake. Prof. Mahalu ameishi kusudio lake la kuitumikia jamii. Nasi kwa kila mmoja wetu aishi kusudio lake, ikiwamo kuitendea mema jamii na msaada," alisisitiza.

Akisoma taarifa ya kumuaga Prof. Mahalu, kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Angela Muhozya, alisema wanamshukuru Mungu kwa maisha yake kwa kuwa alitimiza maono ya kuanzishwa kwa taasisi ya matibabu ya moyo nchini.

Alisema kwa kipindi alichokuwa anaugua ikiwamo kupatiwa matibabu nchini India kwenye hospitali ya Apollo hadi aliporejea nchini kupatiwa matibabu JKCI, wanataaluma walipata fursa ya kuagana naye, ikiwamo kuachiwa wosia wa namna ya kuendeleza taasisi hiyo.

"Tulipata nafasi ya kumuuguza na ametuachia wosia. Tunamuomba Mungu atusaidie kuendelea kuishi maono yake, pengo lake halizibiki. Mungu atusaidie kuliziba pengo lake," alisema Dk. Muhozya.

Jaji Warioba akitoa salamu za rambirambi, alisema Prof. Mahalu alikuwa rafiki, ndugu na mtu wa karibu kati ya familia mbili, ikiwamo kusoma pamoja kwenye shule tofauti miaka ya 1950.

"Tumekuwa karibu tangu tukiwa watoto akiwa na miaka 14, mimi nikiwa na miaka 17. Kwenye mitihani ya kidini Shule ya Sekondari Bwiru alifanya vizuri alikuwa na akili na aliongoza.

Kabla hajahamia shuleni hapo niliongoza, alipokuja niliacha kuongeza," alisema Jaji Warioba.

Alisema maisha waliyoishi sehemu tofauti hadi ukubwani, anamtamfsiri Prof. Mahalu kama mtu aliyekuzwa na upendo, mcha Mungu, msaidizi kwa wengine aliyependa kutekeleza jambo hadi likatimia.

"Ninakumbuka nilikuwa mvivu kupiga pasi na yeye alikuwa mvivu kufua tulipokuwa shuleni Tabora. Tulipeana majukumu, yeye anapasi (kunyoosha) nguo na mimi nifue. Pia nilimwambia kana wanafamilia akikwenda kusoma Makerere (Uganda) nitatoa huduma kadhaa kwa mdogo wake yaani Prof. Costa Mahalu.

"Tulikubaliana yeye asome udaktari na mimi nisomee sheria kwa manufaa ya familia lakini naona yeye amehudumia zaidi familia na jamii. Katika ndoa yeye alikuwa msimamizi wangu, nami nikawa msimamizi wake alipofunga ndoa. Tunashukuru Mungu tukisheherekea maisha yake,"alisema.

Prof. Mahalu aliyezaliwa Novemba 14, 1944 alifariki dunia wiki hii akipatiwa matibabu JKCI. Alikuwa Daktari Bingwa wa Moyo akihudumia ndani na nje ya nchi kama Zimbabwe na Uingereza.

Pia alikuwa mwanataaluma Bugando, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya JKCI kwa vipindi viwili mfululizo. Ameacha mjane na walijaliwa kupata watoto wanne na wajukuu saba.

# Ujenzi wa Bwawa la Nyerere kufikia asilimia 91 Septemba

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, amebainisha kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu, ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) utakuwa umefikia asilimia 91.

Akizungumza jana baada ya menejimenti ya TANESCO kutembelea mradi huo, Chande alisema lengo la ziara hiyo ni kufanya tathimini ya mwenendo wa ujenzi na hali ya mvua za vuli zinazotarajiwa kunyesha kati ya Oktoba na Desemba kama ilivyotangazwa na Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Alisema maendeleo ya ujenzi wa mradi huo ni mazuri, huku akiwapongeza wahandisi na wafanyakazi wa shirika hilo wanaousimamia.

"Ukamilikaji wa mradi huu utatuwezesha kuwa na umeme wa uhakika utakaokidhi mahitaji ya uchumi. Timu ya menejimenti ya TANESCO imani yake ni kwamba kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na mchango mkubwa wa kuondoa upungufu wa umeme unaojitokeza katika miezi ya Oktoba na Desemba.

"Mambo yanakwenda na huenda upungufu wa umeme ukawa historia huko tunakokwenda, tutaongeza umakini katika utekelezaji wake," alisema Chande.

Kwa mujibu wa Chande kumekuwa na ongezeko la mahitaji ya umeme hadi kufikia megawati 1,482.7 mwezi huu kutoka megawati 1,354 za mwaka 2022.

Aliifafanisha hatua hiyo na mashindano makubwa ya kutumia umeme kutokana na mahitaji huku TANESCO ikiongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji kwa Watanzania.

"Endapo utabiri huo utakwenda kama ulivyopangwa, bwawa hilo litajaa kwa haraka zaidi. Mvua zikinyesha kama ilivyotarajiwa itakuwa heri, lakini zikiongezeka tumejiandaa kwa kuweka mipango itakayohakikisha kazi za mradi zinaendelea pasipo kupata changamoto," alisema Chande.

Katika kuwaandaa mapema wataalamu watakaoendesha mradi huo, Chande alisema tayari wameshaongeza wafanyakazi 24 kwa ajili ya kujiandaa kuendesha mchakato huo utakapokamilika.

Alisema ili mradi huo uanze kufanya kazi, unahitaji wafanyakazi 221 pindi utakapokamilika. Alisema kwa sasa kuna Zaidi ya wafanyakazi 90 na watakuwa wakiwapeleka kwa awamu kulingana na mradi utakapofikia.

Hata hivyo alisema pamoja na kuhitajika wafanyakazi 221, hawatapelekwa kwa wakati mmoja bali kwa makundi na kwa wakati husika. Alisema kundi lililopo sasa hivi linahusika na utalaamu wa uhandisi mitambo ya umeme.

# Wanafunzi 86,620 wapata udahili vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

WAOMBAJI 86,624 kati ya 116,133 walioomba udahili wa shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo wa 2023/24, wamechaguliwa kujiunga na masomo katika vyuo 80 nchini.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Tanzania (TCUO, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitangaza kumalizika kwa awamu ya kwanza ya udahili na kufungua awamu ya pili.

Alisema kati ya waombaji hao, 29,509 hawajapata udahili huku 43,411 wakidahili chuo kimoja na 43,213 wamedahiliwa zaidi ya chuo kimoja.

Prof. Kihampa alisema katika mwaka wa masomo 2022/23 awamu ya kwanza, waombaji walikuwa 106,295 na waliodahiliwa walikuwa 75,163, wasiodahiliwa 31,132, waliodahiliwa chuo kimoja walikuwa 38,157 na zaidi ya chuo kimoja walikuwa 37,006.

"Katika awamu hii ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2023/24, programu 809 zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na programu 757 mwaka 2022/23. Hili ni ongezeko la programu 52 za masomo," alisema.

Kwa upande wa nafasi za udahili, Prof. Kihampa alisema kwa mwaka huu kuna jumla ya nafasi 186,289 ikilinganishwa na nafasi 172,168 mwaka uliopita ambazo ni ongezeko la nafasi 14,121 sawa na asilimia 8.2 katika programu za shahada za kwanza.

Pia alisema katika awamu ya kwanza ya udahili, waombaji 86,624 sawa na asilimilia 74.6 ya waombaji wote walioomba udahili, wamepata udahili kwenye vyuo walivyoomba.

"Tume inatangaza kuwa awamu ya pili ya udahili imeanza leo (jana) hadi Septemba 6, mwaka huu. TCU inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakutuma maombi ya udahili au hawakupata nafasi za kudahiliwa katika awamu ya kwanza, watumie fursa hii," alisema.

Prof. Kihampa aliwakumbusha waombaji kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja, yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika.

"Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa," alibainisha.

Alisema TCU inawaasa wananchi kuepuka matapeli au wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya namna ya kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu nchini.

"Tume ina mawakala inaowatambua wanaohusika kupeleka wanafunzi vyuo vya nje ya nchi lakini vyuo vya hapa Tanzania hatuna mawakala. Tunawatahadharisha waombaji na tunawaeleza kuwa, maombi yatumwe kidigitali na siyo kujaza kwenye karatasi," alisisitiza Prof. Kihampa.

# Wamachinga wakubali kulipa kodi 100,000/-

**Na Restuta James**

WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu kama machinga, wamekubali kulipa kodi ya Sh. 100,000 kwa mwaka, kiwango ambacho kitalipwa kwa awamu nne. Hatua hiyo imefikiwa baada ya kundi hilo kupewa elimu ya mabadiliko ya sheria za kodi kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Meneja wa TRA Mkoa wa Kikodi Kariakoo, Kabula Mwemezi, alisema baada ya kutoa elimu hiyo ya mabadiliko ya sheria za kodi zilizopitishwa na Bunge la Bajeti, Juni, mwaka huu, wamekubali kulipa kiwango hicho cha fedha.

Alisema watakaolipa ni wale wenye mauzo ya Sh. 4,000,000 na zaidi, ambazo zitalipwa kidogo kidogo kwa kutengeneza namba ya malipo serikalini kwa mfumo wa kielektroniki.

"Mwitikio wenu umenipa hamasa ya kufanyakazi. Tumesikiliza maoni na niseme tu tutaendelea kufanya kazi nanyi kwa karibu ili kwa pamoja tuijenge nchi yetu," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Kamishna wa Kodi za Ndani wa TRA, Edmund Kawamala, alisema wananchi wa ngazi zote wanapaswa kulipa kodi ili serikali iweze kutoa huduma muhimu za kijamii kama elimu, afya, maji na miundombinu zenye ubora kwa wananchi.

"Nia ni kuiwezesha serikali kutekeleza miradi yote ya kimkakati nchini," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wamachinga Kariakoo, Stephen Lusinde, aliishukuru TRA kwa kuwapa elimu na kueleza kwamba wafanyabiashara hao wapo tayari kulipa kodi. "Hakuna hata mmoja wetu ambaye hayupo tayari kulipa kodi, tunachokiomba siku zote ni kututengenezea mfumo ambao utatuwezesha kulipa kodi katika mazingira yetu," alisema. Alisema awali wamachinga walikuwa wanagombana na TRA kwa kuwa mamlaka hiyo ilitaka iwape mashine za EFD, akieleza hazikuwa rafiki kwao. "Si haki wamachinga tupite bure kwenye barabara nzuri na watoto wetu wasome bure. tunatamani sana tushiriki kikamilifu kuijenga nchi yetu na nikuhakikishie kwamba hawa unaowaona hapa wote wako tayari kulipa kodi," alisema.

Baadhi ya wamachinga waliozungumza katika mkutano huo waliiomba TRA kupata maoni yao kabla haijatunga sheria ya kodi. Mchuuzi wa viungo, Raibu Omari, alisema maoni ya kundi hilo yatazisaidia mamlaka kutunga sheria rafiki ambazo zitatekelezwa kwa urahisi na watu wa kada zote. "Ushirikishwaji ndiyo njia rahisi kabisa. Lakini pia mfumo, wamachinga wakiwekewa njia rahisi ya kulipa hata Sh. 1,000 kila siku tutalipa, lakini siyo EFD," alisema.

"Baada ya elimu hii, tuko tayari kulipa kodi TRA ili tupate dawa kwenye hospitali zetu, tujenge barabara na watoto waende shule," alisema mchuuzi wa vijora, Ummy Juma.




Meneja wa Sekta isiyo rasmi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Rehema Chuma (kushoto), akimsikiliza kwa makini Katibu wa UVCCM Mkoa wa Tanga, Theresia Makyao, alipotembelea banda la mfuko huo, wakati wa kongamano jijini Tanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa majitaka kukamilika Septemba

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa majitaka wa maeneo ya PSSSF Sinza-Kijitonyama jijini Dar es Salaam, unatarajiwa kukamilika mwezi ujao na utagharimu shilingi bilioni 1.4

Wasimamizi wametakiwa kuongeza nguvu na kufanya kazi usiku na mchana ili mradi uweze kukamilika mapema iwezekanavyo na kunufaisha wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu, alipotembelea kuona maendeleo ya mradi huo.

Utekekelezaji wa mradi huo ambao sasa umefikia asilimia 18 utakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa maeneo hayo utakapokamilika.

"Mradi huu ni wa kimkakati, wenye lengo la kuwasaidia wafanyabiashara waliopanga kwenye jengo la PSSSF, pamoja na wananchi wa maeneo ya Sinza na Kijitonyama ambao ardhi yao ina kiwango cha juu cha maji (water table) hivyo kusababisha uchafuzi wa Mazingira mara kwa mara," alisema Kingu.

Aidha, Kingu aliagiza kazi hiyo ifanyike usiku na mchana na kuongeza vitendea kazi ili mradi ukamilike ndani ya muda uliopangwa ambao ni mwezi Septemba badala ya Oktoba mwaka huu.

Naye msimamizi wa mradi huo, ambaye ni Mkurugenzi wa Usafi wa Mazingira wa DAWASA, Mhandisi Lydia Ndibalema, alisema wamepokea maelekezo ya Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu na mradi utakamilika kwa wakati.

"Mradi huu utakamilika ndani ya muda, tumejipanga kama idara na Afisa Mtendaji Mkuu ametuongezea vitendea kazi ili kazi iende kwa kasi na kuanzia kesho mabadiliko yataonekana," alisema.

Aidha, alisema mradi huo unagharimu shilingi bilioni 1.4 na utanufaisha zaidi ya wateja 1,000 na kumaliza changamoto ya uchafuzi wa Mazingira katika eneo hilo la Sinza na Kijitonyama.

Mradi wa Usafi wa Mazingira PSSSF Sinza-Kijitonyama utanufaisha maeneo ya Sinza B, Sinza C, Mabatini pamoja na Kijitonyama.

# NSSF yatoa elimu kongamano ununuzi

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umeshiriki na kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa washiriki wa kongamano la Wanawake na Ununuzi wa Umma, linaloendelea jijini Tanga.

Meneja wa Sekta Isiyo Rasmi wa NSSF, Rehema Chuma, akitoa mada katika kongamano hilo lililoanza Agosti 23, mwaka huu, alisema kupitia kongamano hilo NSSF imetoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Kwa mujibu wa Chuma, sekta hiyo imebeba kundi kubwa kama vile wakulima, wafugaji, wavuvi, mama lishe, bodaboda na wajasiriamali na wengine wote, hivyo elimu inahitajika ili kuwawezesha kujiunga na kuchangia katika mfuko kwa maisha yao ya sasa na baadae.

Lengo la kongamano hilo ni kueleza fursa za biashara zinazoambatana na mradi wa bomba la mafuta Afrika Mashariki (EACOP), hivyo mradi huo ni fursa kwa NSSF kupata wanachama wapya ambao watapata ajira za moja kwa moja na wale watakaonufaika na ajira za muda.

Wanufaika wengine katika mradi huo ni mama lishe na baba lishe pamoja na bodaboda ambao wanaweza kujiunga na kuchangia katika mfuko.

Meneja huyo aliwahamasisha wanawake kuchangamkia fursa za mradi wa bomba la mafuta pamoja na kujiunga na kuchangia katika mfuko ili kujiwekea akiba yao kwa Maisha ya sasa na ya baadaye.

Katika kongamano hilo, NSSF licha ya kutoa elimu ya hifadhi ya jamii, pia itaeleza fursa mbalimbali zinazopatikana zikiwamo za nyumba na viwanja ambazo zinauzwa kwa bei nafuu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF iweke wazi vigezo vya tuzo ya mfungaji bora ligi kuu

**LIGI** Kuu Tanzania bara imeanza, na tayari timu nyingi zimeshacheza mechi za mzunguko wa pili kasoro timu chache ambazo zimecheza mzunguko mmoja pekee.

Kuanza kwa ligi Agosti 15 ni mwanzo wa kusaka tuzo mbalimbali za binafsi kwa wachezaji wote wanaoshiriki ligi hiyo ya NBC.

Kwa mfano kuanza kwa ligi tayari kumefungua mbio za kusaka tuzo ya mfungaji bora wa ligi kuu kwa msimu huu baada ya msimu uliopita tuzo hiyo kuchukuliwa kwa pamoja na wachezaji wawili, Saido Ntibazonkiza wa Simba na Fiston Mayele ambaye alikuwa Yanga.

Wachezaji hao wote walikuwa na mabao 17 na kufungana kwa idadi ya mabao na kupelekea kamati ya tuzo ya Shirikisho la soka nchini (TFF) kuamua kutoa tuzo kwa wachezaji wote wawili.

Hata hivyo tuzo hiyo ilileta mvutano mkubwa na kuibua maswali mengi kwa wadau wa soka kutokana na namna maamuzi ya kugawana yalivyochukuliwa.

Kimsingi minong'ono ilianza baada ya TFF kuchukua muda mrefu kutoa maamuzi ya nani anastahili kupata tuzo hiyo baada ya wachezaji wawili kufungana kwa idadi hiyo ya magoli.

Wengi waliamini atakayechukua tuzo hiyo ni yule ambaye licha ya kuwa na mabao mengi lakini ana idadi kubwa ya 'assist', hata hivyo hiyo haikuwa kigezo, na wapo waliokuwa wanaamini yule ambaye ana mabao machache aliyofunga kwa penalti ndiye angechukua tuzo hiyo, hata hivyo haikuwa hivyo.

Sintofahamu hiyo ilitokana hasa na kamati ya tuzo ya TFF kutoweka mapema vigezo na kanuni ndogondogo ya kuamua nani anastahili kupewa tuzo hiyo pale wachezaji zaidi ya mmoja wanapokuwa na mabao mengi yanayolingana mwisho wa msimu.

Ni vyema sasa mwanzoni mwa ligi hii TFF wakaweka vigezo na kanuni za kuamua mfungaji bora pale wachezaji zaidi ya mmoja wanapokuwa wamefungana kwa idadi ya mabao mengi kwenye ligi.

Hii itasaidia kuondoa sintofahamu ya kujua nani atakuwa mchezaji bora kati ya wachezaji wawili au zaidi waliofungana kwa ufungaji.

Kukiwa na vigezo na kanuni za wazi kila mmoja atajua nani ni mfungaji bora na kutaondoa ile dhana ya upendeleo kwa baadhi ya wachezaji kutoka kwenye timu kubwa.

Hakuna sababu ya kuwa na usiri kwenye maamuzi ya nani anastahili kuwa mfungaji bora wa ligi baada ya ligi kumalizika, TFF kupitia kamati husika inapaswa iweke kanuni za wazi za kuamua nani mchezaji bora pale wachezaji wanapofungana kwa idadi ya magoli.

Kwa mfano baada ya wachezaji wawili kufikisha idadi ya juu ya mabao ya kufunga na kulingana, basi wanaweza wakaweka kanuni kuwa kama ikitokea hivyo wataangalia nani amechangia mabao mengi kwenye timu 'Assist', au waweke kigezo kingine kitakachotoa ukakasi kwenye maamuzi.

Hizi ni kasoro zilizoonekana kwenye utoaji tuzo msimu uliopita na Nipashe tunaamini kamati husika itafanyia kazi mapema na kuja na kanuni za wazi zitakazojulikana kwa wadau wa soka za namna gani mfungaji bora anapatikana pale kunapokuwa na wachezaji zaidi ya mmoja wanaokuwa na magoli sawa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mabao 29 Ligi Kuu matatu tu ya vichwa, kuna tatizo sehemu

Na Adam Fungamwango

**KATIKA** mabao 29 yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, matatu tu yamefungwa kwa kutumia vichwa.

Ina maana mabao 26 yamefungwa kwa njia nyingine ya mguu wa kushoto au kulia, na matatu ndiyo wafungaji wametumia vichwa.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, wachezaji waliofunga kwa vichwa ni Elius Maguri akifanya hivyo kwenye mechi ambayo timu yake ya Geita Gold ilicheza dhidi ya Ihefu, Agosti 15 na kuifanya kuondoka na ushindi wa bao 1-0 ikiwa ugenini,

Feisal Salum wa Azam akifanya hivyo kwenye moja kati ya mabao yake matatu Agosti 16 ilipocheza dhidi ya Kitayosce na kushinda mabao 4-0 ikiwa nyumbani.

Bao lingine la kichwa lilifungwa na Fabrice Ngoma wa Simba Agosti 17, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, ikipata ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya wenyeji Mtibwa Sugar.

Katika hili tunaona kuna udhaifu mkubwa sana katika mabao ya vichwa kwenye Ligi Kuu na hapo ndipo tunaanzia kutafuta tatizo lipo wapi.

Binafsi kwanza kabisa nasema timu zetu zina matatizo sana kutumia mipira iliyokufa, yaani kupiga faulo ambazo zinaelea katikati ya kipa kwa wachezaji wa timu zote mbili.

Wapiga mipira hiyo kwa sasa ni adimu sana, ingawa kuna wachache ambao wanaweza kupiga faulo za moja kwa moja.

Wachezaji wanaopiga faulo la uchonganishi ni muhimu sana kwani wanasababisha kufungwa mabao ha sa la vichwa.

Tatizo lingine ni kwamba huenda wachezaji wengi wa Kitanzania, na hata wale wanaokuja nchini kucheza soka la kulipwa ni waoga kupiga vichwa.

Ili kufunga mipira ya vichwa ni lazima mtu ajitose, apige mpira ulio juu kuelekea golini na ili awe na shabaha ni lazima awe amefumbua macho.

Hata wale wanaopiga vichwa mara nyingi utaona vichwa vyao vinakwenda nje, lakini ukichunguza ukweli utakuta walikuwa wamefumba macho.

Mchezaji anapofumba macho hawezi kupiga mpira kwa usahihi kwani mpira ndiyo unagonga kichwa na mchezaji na si mchezaji anapiga mpira.

Inawezekana pia hata wapiga krosi wenyewe nao ni tatizo, wanapiga ambazo hazina macho, au maeneo ambayo si sahihi.

Nchi yetu pia kwa sasa haina wachezaji wapiga vichwa wazuri kama ilivyokuwa zamani kina Abeid Mziba, Edward Chumila, John Makelele 'Zig Zig,' Mohamed Bob Chopa, Peter Tino, Zamoyoni Mogella na wengine wengi ambao walikuwa wakisifika kwa kufunga mabao ya vichwa.

Udhaifu wa wachezaji wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara hupiga vichwa mipira hasa wanapokuwa kwenye kundi la watu wengi unadhihirishwa hata zinapocheza mechi za kimataifa.

Timu za Simba na Yanga kwa miaka kadhaa nyuma zimekuwa zikiadhibiwa sana na klabu kutoka nje ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kwa mipira ya kutengwa.

Mara nyingi ndiyo mipira ambayo mabao wanafungwa kwa vichwa. Udhaifu ambao upo kwenye Ligi Kuu wa kufunga mabao kwa vichwa mpaka sasa kwa wachezaji ndiyo upo hata kwa mabeki wa timu za Bongo zinapocheza michuano ya kimataifa.

Hii inaonyesha kuwa kuna woga wa wachezaji kupiga vichwa kwa usahihi pale mpira unapopigwa katikati ya msitu wa wachezaji.

Mastraika wanaogopa kupiga ili kufunga na mabeki wanaogopa kuokoa. Haileti athari sana kwa sababu kwenye ligi yetu wanakutana waoga kwa waoga, lakini likija suala la mechi za kimataifa, udhaifu upande wa ushambuliaji unaonekana, lakini udhaifu kwa mabeki unaonekana kwanza mastaika wa timu pinzani hutumia sana mwanya huo kuziadhibu timu za Tanzania.

Wito kwa makocha wa timu mbalimbali za Ligi Kuu kuanza kuliangalia hilo kwani ligi yetu imekuwa ikiangaliwa sana na nchi mbalimbali kwa sasa.

HABARI KITAIFA

# Serikali kutatua kero utozaji kodi katika vifaa tiba na dawa

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imesikia kilio cha kampuni, hospitali zinazotoa huduma ya afya nchini kuhusu kutozwa kodi pindi wanapoagiza vifaa tiba na dawa kutoka nje, ikisema imeanza kuchukua hatua ikiwamo kukutana na mamlaka husika ili kuondoa kadhia hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua maonyesho ya pili ya kimataifa ya utabibu na maabara yaliyoshirikisha kampuni zaidi ya 100 kutoka ndani na nje ya Tanzania.

"Nimesikia kilio chenu kwamba, huwa mnatozwa kodi kipindi mnapoagiza vifaa tiba na dawa kutoka nje. Muda mwingine mnavutana na mamlaka husika (TRA) kuhusu vifaa hivyo kwamba vingine siyo vifaa tiba hali inayosababisha kutozwa kodi bandarini," alisema Dk. Mollel.

Dk. Mollel alisema serikali inatambua umuhimu wa kampuni za kuzalisha na kuuza vifaa tiba na dawa nchini zilivyo na umuhimu katika ukuzaji uchumi, hivyo itakuwa nazo bega kwa bega katika kuwasaidia. Alisema katika kuhakikisha kunakuwapo na usawa, haki na kuondoa malalakio katika sekta ya afya atafanya kikao na viongozi wa Bohari Kuu ya Dawa ( MSD), Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya ili kutatua kero zilizopo.

Dk. Mollel alisema: "Serikali inafahamu changamoto zinazowakabili. Hivyo tutakwenda kuzitatua kwa sababu mnachangia sana huduna za afya hapa nchini".

Naye Naibu Balozi wa India nchini, Manoj Vernan, alisema maonyesho hayo ni mwendekezo wa ushirikiano kati ya Tanzania na India uliodumu kwa zaidi ya miaka 50.

Alisema vifaa tiba na dawa zinazozalishwa na kampuni kutoka India ni kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania kwenye kusaidia sekta ya afya.

"Hospitali za India zina uhusiano na hospitali za Tanzania katika kutoa matibabu na mafunzo. Ushirikiano huu uliwekwa na waasisi wa mataifa haya," alisema Vernan.

Rais wa Chama cha Wafamasia Tanzania (TPS), Fadhil Hezekiah alisema lengo la maonyesho hayo ni kuwavutia wawekezaji kujenga viwanda vya kuzalisha dawa nchini. Alisema waagizaji dawa nchini wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kutozwa kodi kwa vifaa, vifaa tiba na dawa zinazozalishwa nchini kuwa ghali kuliko zinazotoka nje ya nchi pamoja na kutokuwapo kwa bei elekezi ya vifaatiba na dawa.



Mratibu na Mwanzilishi wa Shule ya Peninsula English Medium (PEMS), Winnie Mlay (katikati), akisaidiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Sally Dawit (wa nne kushoto) na mwanafunzi Suzana Badi kukata keki ikiwa ni sehemu ya kusherehekea mahafali ya 19 ya darasa la saba ya shule hiyo, Masaki Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI.**

# Ujenzi madaraja kwa mawe wapunguza gharama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, amesema teknolojia mbadala ya matumizi ya mawe katika ujenzi wa madaraja umesaidia kupunguza gharama kwa asilimia 50.

Mhandisi Seff alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wakala na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema hadi Machi, mwaka huu, TARURA imejenga madaraja 163 ya mawe yenye thamani ya Sh. bilioni 8.7 ambapo gharama imepungua kwa

zaidi ya asilimia 50. Madaraja hayo yamejengwa katika mikoa ya

Kigoma (92), Singida (24), Tabora (Matano), Kilimanjaro (10), Mbeya (mawili), Arusha (sita), Morogoro (mawili), Rukwa (matatu) , Pwani (moja), Ruvuma (matatu) na Iringa 15.

Pia TARURA inaendelea kufanya majaribio ya teknolojia mbalimbali ili kutumia udongo ulioko eneo la kazi badala ya kusomba kutoka maeneo mengine ya mbali.

"Teknoloia hizo ni pamoja na ECOROADS, Ecozyme, na Geo-Polymer. Hadi sasa kwa kutumia Teknolojia ya ECOROADS katika jiji la Dodoma imejengwa kilomita moja ambayo imekamilika na katika wilaya ya Mufindi zitajengwa kilomita 10 na mkandarasi yupo kwenye matayarisho ya kuanza kazi," alisema.

Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wakala, alisema katika mwaka wa fedha 2023/24 barabara zenye kilomita 21,057.06 zitafanyiwa matengenezo na kilomita 427 zitajengwa kwa kiwango cha lami.

"Kilomita 8,775.62 zitajengwa kwa kiwango cha changarawe, madaraja na makalavati 855 yatajengwa na mifereji ya mvua kilomita 70," alisema.

Alisema Sh.bilioni 858.517 zimeidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara za wilaya.

"Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 710.31 ni za ndani na Sh. bilioni 148.207 ni za nje kupitia miradi ya RISE, TACTIC, Bonde la Mto Msimbazi na mradi wa Agri Connect," alisema.

Pia alisema, wakala umetangaza kazi za ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara zaidi ya asilimia 60 ya mpango wa mwaka 2023/24 ambapo baadhi ya kazi utekelezaji umeanza.

Alisema jukumu kubwa la TARURA ni kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya mtandao wa barabara za wilaya.

"Utafiti unaonyesha kuwa maeneo ya kilimo vijijini yakiwa yanafikika kwa mwaka mzima, inaongeza ukuaji wa kilimo na kupunguza umasikini na hasa ukizingatia takribani asilimia 65.1 ya watanzania wanaishi vijijini na sekta ya kilimo kwa Tanzania inachangia pato la taifa kwa takribani asilimia 26.

"Hii inadhihirisha umuhimu wa barabara za vijijini chini ya TARURA zinazopitika misimu yote ya mwaka katika kuchangia ukuaji wa Kilimo na kupunguza umaskini," alisema.

Alisema kwa msingi huo serikali imeiongezea TARURA bajeti yake mara tatu zaidi ikiwa ni kuendeleza juhudi za awamu zilizopita za kuboresha barabara za vijijini.

"Kama mnavyojua kwa sasa tuko kwenye utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Pili tangu kuanzishwa kwa TARURA mwaka 2017 tukiwa na lengo ifikapo mwaka 2025 angalau asilimia 85 ya barabara za wilaya ziwe zinapitika kwa misimu yote," alisema Mhandisi Seff.

# NHC yasisitizwa kasi kudai madeni

**Na Munir Shemweta,** WANMM

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii, imelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kutilia mkazo ukusanyaji madeni ya wapangaji katika nyumba zake.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Timetheo Mnzava, amesema pamoja na shirika hilo kujitahidi katika ukusanyaji malimbikizo ya kodi kutoka kwa wapangaji, bado linatakiwa kuongeza kasi ya ukusanyaji madeni.

Akizungumza wakati wa kikao cha kupokea taarifa ya utendaji kazi wa NHC jijini hapa juzi, Mnzava alilitaka pia shirika hilo kuweka msisitizo zaidi katika kuzuia kuzalisha madeni badala ya kusubiri mpaka wapangaji kuwa na malimbikizo makubwa ya madeni.

Aidha, wajumbe wa kamati hiyo walitaka kuwapo mikakati madhubuti itakayowafanya wapangaji kulipa kodi kwa wakati.

Vile vile, kamati hiyo imeonyesha kuridhishwa na utendaji kazi wa shirika hilo katika kutekeleza miradi yake na kulitaka kuangalia namna ya kujenga nyumba za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi.

"Niipongeze NHC pamoja na Wizara ya Ardhi maana kazi za shirika zinaonekana hata kwa macho. Nisisitize muweke jitihada pia katika ukarabati wa nyumba zenu ili wapangaji wakae vizuri," alisema mjumbe wa kamati, Cecilia Paresso.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza mbele ya kamati hiyo, alisema kwa sasa upo uhitaji mkubwa wa nyumba na serikali iko katika marekebisho ya sera ili kuwezesha ushiriki wa taasisi na sekta binafsi katika uzalishaji nyumba.

"Kama serikali tutahakikisha kasi ya ujenzi wa nyumba inaongezeka maana takwimu za sensa ya watu na makazi zimeonyesha uhitaji mkubwa wa nyumba na uzalishaji ukiwa mdogo, hivyo msisitizo ni kuzalisha nyumba za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi," alisema Dk. Mabula.

# AGRA yataja mambo nane kuinua kilimo

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), imetoa mapendekezo nane ambayo serikali na wadau wa kilimo wanapaswa kuyafuata ili kufikia lengo la kulisha Afrika.

Vipaumbele hivyo ni kujenga mifumo endelevu kwa wakulima, kupata soko la mazao yao nje ya nchi, kufanya kilimo endelevu, kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora, sera nzuri za kilimo, kufanya kilimo endelevu, kutanua masoko na ushirikishwaji kwenye kilimo cha faida.

Meneja wa taasisi hiyo Tanzania, Vianey Rweyendela, alivitaja vipaumbele hivyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa semina ya kuwajengea uwezo waandishi na wahariri kuhusu masuala ya kilimo.

Pamoja na mambo mengine, aliwataka wakulima kutumia mbegu bora ili kujiongezea kipato na kunufaika na kilimo, akisistiza mkulima anapotumia mbegu bora anakuwa yupo kwenye asilimia 40 ya kupata kipato kikubwa.

Alisema: "Ukitumia tu mbegu bora, unajiweka kwenye asilimia 40 ya kupata kipato kizuri, hapo bado hujaongeza maoni ya wataalamu, hujaweka mbolea wala kupiga dawa"

Aliongeza: "Kwa hiyo, utaona ni kwa kiasi gani mtu anayetumia mbegu bora anaweza kupata kipato kikubwa tofauti na asiyetumia".

Rweyendela ambaye pia ni mtaalamu wa mbegu alishauri elimu itolewe kwa wakulima akisema wengi wao wanatabia ya kugeuza nafaka kuwa mbegu, jambo ambalo linachangia kupata kipato kidogo.

Alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa kuhabarisha umma kuhusu sekta ya kilimo, akiwataka kutumia nafasi zao kuisaidia jamii inayohitaji kujua mambo mengi kuhusu sekta hiyo.

Alisema: "Wakulima wengi hawana uelewa juu ya mbegu bora, wengi wanaangamia kwa kununua mbegu feki, lakini sasa hivi anaweza akaihakiki kabla ya kuipeleka shambani na kujiridhisha kama ipo sawa kwa kutumia T-hakiki".




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo wa Benki ya Exim Andrew Lyimo (katikati), Mkurugenzi wa Indesso, Feri Agustain (kulia) na Desdery Rutta, Mshirika wa kampuni ya Amani Essence (kushoto) wakionyesha makubaliano ya ushirikiano wakati wa Kongamano la Biashara kati ya Indonesia na Tanzania, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kongamano la ushirikiano China na Afrika Mashariki kufanyika UDSM

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu, anatarajiwa kufungua Kongamano la Kimataifa la kusherehekea miaka 10 ya ushirikiano baina ya nchini za Afrika Mashariki na China, litakalowakutanisha washiriki 180 kutoka nchi hizo. Kongamano hilo litafanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa siku mbili kuanzia leo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF), Joseph Butiku alisema ushirikiano wa China na Afrika Mashariki unatekelezwa kupitia Mpango wa Ukanda Mmoja, Njia Moja (BRI) ambao una lengo la kuchochea amani, umoja na maendeleleo kwa nchi husika.

Alisema baada ya ufunguzi kutakuwa na uwasilishaji wa mada mbalimbali za kuelezea namna BRI ilivyofanya kazi kwa miaka 10 na namna ya kwenda mbele.

Butiku alisema kongamano hilo limeandaliwa na MNF kwa kushirikiana na Ubalozi wa China, hivyo linakwenda kukidhi hitaji la nchi husika.

Alisema China inatumia BRI kuhakikisha kila upande unanufaika, kwani historia inaonesha nchi hiyo imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa nchi husika.

Akitolea mfano, Butiku alisema Tanzania imenufaika kwa kushirikiana na China katika eneo la elimu, afya, kilimo, miundombinu, alitaja mradi wa ujenzi wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), jengo la makao makuu ya MNF, Chuo cha Siasa Kibaha na Bunge la Tanzania.

"China miaka yote wamekuwa marafiki tukishirikiana kwa shida na raha katika masuala ya kilimo, nguo, viwanda, uzalishaji, ulinzi, miundombinu na hata kupigania uhuru,"alisema.

Alisema China imekuwa ikihitaji kuwepo kwa dunia yenye amani, umoja na maendeleo kwa watu wote na hilo limedhihirika kwao kwani hawajawahi kutamani utawala mwingine na wamekuwa wakifanya biashara zao kwa amani.

Butiku alisema anatamani kuiona dunia ikiendelea kuwa na amani na kuwepo shughuli za kiuchumi kwa maendeleo ya watu wake, kama China inavyofanya.

Mwenyekiti huyo alisema kongamano hilo litajadili pia mambo yanayoendelea kati ya Tanzania na China, mafanikio na changamoto walizozibaini ndani ya miaka hiyo na kupendekeza namna ya kupata ufumbufuzi.

Butiku alisema watoa mada wataeleza maendeleo yaushirikiano huo wa mpango wa BRI, kwa nchi za Afrika Mashariki na kuainisha maeneo mengine yanayohitaji msukomo zaidi wa ushirikiano ili kuhakikisha maendeleo yanawafikia wananchi wa mataifa hayo.

# Msalato Satellite City' kuwa mji wa mfano

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema mradi wa Kupanga na Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika eneo la Kitelela mkoani Dodoma, maarufu kama Msalato Satelite City, utakuwa wa mfano kwa matumizi mbalimbali.

Wizara inatekeleza mradi kwa kutwaa eneo katika mtaa wa Kitelela lenye ukubwa wa takriban ekari 971 kwa kulipa fidia, kupanga na kupima eneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali na viwanja 1,012 vimepimwa.

Akizungumza wakati akiwasilisha taarifa ya wizara kuhusu Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii juzi jijini Dodoma, Dk. Mabula alisema katika mradi huo, huduma mbalimbali zinapatikana sambamba na kuzuia ujenzi holela.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma katika utekelezaji Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali katika jiji hilo.

"Suala la Kitelela, tunataka mradi huu uwe wa mfano. Tunataka mradi usimamiwe na uwe tofauti na miradi mingine," alisema Dk. Mabula.

Alibainisha kuwa utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma unaendana na malengo yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kupanga na kupima viwanja 2,500,000 kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2020.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga, alisema kupitia mradi huo wa Kitelela, fedha zitakazopatikana zinatarajiwa kuzungushwa kwa kuanzisha miradi mipya kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Mradi wa Kitelela tunaufanya kama 'demo' (mfano) na fedha zinazopatikana kupitia mradi huo zitumike kutwaa na kupima maeneo mengine. Hii ni moja ya mikakati ambayo wizara inaendelea nayo," alisema Sanga.

Awali, wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii walipongeza wizara katika kutekeleza mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

Hata hivyo, waliitaka wizara kudhibiti mapema ujenzi holela badala ya kuacha na kusubiri kufanya urasimishaji makazi.

"Naipongeza wizara kwa namna ilivyojipanga lakini ni vizuri ikawa 'pro- active' hasa kwa ile miji inayokuwa na tabia ya kuacha kusubiri kurasimisha makazi." alisema mjumbe wa Kamati, Shaaban Shekilindi, ambaye ni Mbunge wa Lushoto.

Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, alisema wizara kwa sasa iko kazini na wajumbe wa kamati hiyo wanapaswa kuiamini katika masuala mbalimbali inayotekeleza.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imewasilisha taarifa zake mbili za utekelezaji mapendekezo ya Kamati Maalum ya Mawaziri Wanane wa Kisekta juu ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 na Utekelezaji wa Program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.





# Waziri ahimiza mafunzo ufundi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema elimu na mafunzo ya ufundi stadi inahitajika ili kuimarisha uwezo wa vijana kujiajiri na kuajiriwa.

Aidha amewataka wahitimu wa mradi wa kukuza ajira kwa vijana Tanzania (E4DT) kuwa na ujasiri na kujiamini kutumia ujuzi wao na kuanzisha miradi yao wenyewe ili wajikwamue kiuchumi.

Mradi huo unafadhiliwa na Shirikisho la Ujerumani la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norway (NORAD), Umoja wa Ulaya (EU), na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea (KOICA) huku ukisimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Shirika la maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Akizungumza jana kwenye kongamano la ajira, Mavunde alisema mafunzo hayo ni hatua muhimu katika kuwawezesha vijana kupata ajira au kujiajiri wenyewe, kuwa wajasiriamali na kuwa sehemu ya kuleta mabadiliko chanya kiuchumi na kijamii nchini.

"Ni wazi kwamba mtu aliyepata ujuzi ana uwezo wa kujikimu akipata taarifa sahihi na kufanya kazi kwa bidi. Niwaombe wafadhili waendelee kutoa fursa za mafunzo kwa vijana wengi zaidi kwani hii imeamsha ari kubwa kwa vijana kupata ujuzi na kujikwamua kiuchumi," alisema.

Alibainisha kuwa Tanzania ina fursa nyingi za ujasiriamali na mahitaji makubwa katika soko la ajira na hivyo mafunzo hayo yamewezesha vijana kupata ujuzi unaohitajika katika sekta mbalimbali za viwanda, ujenzi, na teknolojia.

"Hii ni fursa nzuri ya kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kujenga ajira kwa wengine. Hivyo, nendeni mkatumie ujuzi wenu vizuri na mkawe mabalozi wa mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa kwenye vyuo vya ufundi nchini," alisema.

Aliomba waajiri kuwatumia vijana wenye ujuzi kwa kuwapatia fursa za kazi na mafunzo ili kuchangia ukuaji wa biashara.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu n Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), CPA Anthony Kasore, alisema mradi huo una lengo la kuongeza ujuzi wa vijana na kuwapa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira.

Alisema shabaha ni kuwafikia vijana 4,000 katika fani za 'Mechatronics', uchomeleaji viwandani, pamoja na ufundi bomba majumbani na viwandani hadi sasa 3,258 wamehitimu.

"Katika mradi huu, walengwa wanapata fursa ya kushiriki mafunzo maalumu ya ujasiriamali yanayoambatana na shindano la kuwapata washindi ambao wataweza kuatamiwa na hatimaye kujiajiri.

Zaidi ya walengwa 600 watapata fursa ya kushiriki mafunzo na kati yao washindi 60 wataweza kuatamiwa na hatimaye kuwezeshwa kujiajiri," alisema.

# Tume yataja mikakati maendeleo TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya TEHAMA (ICTC) imetaja mikakati ya kukuza uchumi wa kidijitali ikiwamo kuhakikisha vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vinazalishwa Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akieleza utekelezaji wa majukumu na mwelekeo wa mwaka 2023/24.

Alisema hatua hiyo itafikiwa kupitia vituo vya ubunifu vitakavyoanzishwa kwenye mikoa nane ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Tanga, Lindi, Mbeya na Zanzibar.

"Vituo vitasaidia mikoa kupambana vizuri katika uchumi wa kidijitali kwa Tanzania, lengo ni kupata wabunifu ambao watatengeneza ajira na kuongeza pato la mkoa. Tumeona kuna kampuni nyingi za Dar es Salaam zinaitwa kutoa huduma kwenye mikoa mingine," alisema.

Alisema uchumi wa kidijitali ni sehemu ambayo inatengeneza fedha nyingi kwa haraka hasa kwa vijana na inachangiza sekta nyingine za kiuchumi kufanya kazi vizuri na kuchochea pato la taifa.

Alibainisha kuwa uchumi wa kidijitali nchini unashikiliwa kwa kiwango kikubwa na mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya.

"Kuna kampuni kubwa za Tanzania zimetengeneza mitaji mikubwa duniani na zinafanya kazi kwenye nchi mbalimbali ikiwamo Nara," alisema.

Alisema mwaka 2022/23 wameanza kujenga kituo cha ubunifu kikubwa kitakachokuwa Dar es Salaam na kitafanya kazi ya kutoa huduma kwa wataalamu, watafiti na wabunifu wa TEHAMA.

Kuhusu teknolojia ya akili bandia, Dk. Mwasaga, alisema tume inashirikiana na baadhi ya vyuo vikuu nchini kuwa na kituo cha kuchakata taarifa zinazohusiana na masuala ya kijiografia ambacho awali kilikuwa Finland ili kukuza uchumi wa data.

"Katika mabadiliko haya ya kidijitali kitu ambacho kinatakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka sana ni akili bandia na inahitajika data, kituo kitachagiza kuwa na uwezo mkubwa kwenye eneo hilo,"alisema.

Alisema wataalam 343 wa TEHAMA wameongezewa ujuzi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo akili bandia.

Katika hatua nyingine, alisema kampuni ndogo za TEHAMA nchini kwa mwaka 2021 zimezalisha mitaji Dola za Marekani milioni 92 na mwaka 2022 wametengeneza mitaji ya Dola za Marekani milioni 80 huku akisema dhamira ya serikali ni kuwa na bunifu nyingi.

Pia alisema Tanzania ni nchi ya nane Afrika kwa kuwa na bunifu zinazozalisha mitaji na kwa Afrika Mashariki inashika nafasi ya pili.

Awali, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema serikali imeamua kuwekeza kwa nguvu kwenye Tanzania ya kidijitali na tume hiyo inasimamia azma hiyo.

"Kuna nchi uchumi wa kidijitali umewafikisha mbali sana kama Marekani masuala ya TEHAMA yanachangia kwa asilimia 10," alisema.



Mwenyekiti wa soko la Sabasaba, jijini Dodoma, Athumani Makole (kushoto), akizungumza kwenye mkutano wa wafanyabiashara uliojadili na kutatua kero mbalimbali sokoni hapo jana. Waliokaa (kutoka kulia) ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Alhaji Adam Kimbisa, Mkuu wa wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabir Shekimweri na Mbunge wa Dodoma, Athony Mavunde. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sera wenye ulemavu yafanyiwa mapitio

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeanza kufanya tathmini na mchakato wa mapitio ya Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuzingatia mlengo wa kijinsia.

Akifungua kikao cha wadau cha kupitia taarifa ya awali ya mapitio hayo jana jijini hapa, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema mapitio hayo yanafanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake (UN WOMEN) huku akitaka yazingatie uwakilishi wa makundi yote ya watu wenye ulemavu ili kuwa na sera bora.

"Ofisi yangu itahakikisha sera hii inakamilika mapema kwa kuwa imekuwa ni maombi ya muda mrefu kwa watu wenye ulemavu kufanyika mapitio haya, naomba timu itakayokwenda kukusanya maoni izunguke kila mkoa na kufika kwenye halmashauri kupata maoni ya watu wenye ulemavu yatakayosaidia kuwa na sera nzuri inayokidhi mahitaji ya sasa," alisema.

Naye Mwakilishi wa UN WOMEN, Jacob Kayombo, alisema shirika limeridhishwa na hatua iliyofikiwa ya mchakato huo na kwamba wanaamini itakamilika kwa wakati.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Jonas Lubago, aliishukuru serikali kwa kutimiza ahadi ya kufanya maboresho ya sera hiyo na kuahidi watashiriki kikamilifu ili kuwa na maboresho mazuri ya sera.

Awali, Mshauri Elekezi ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Consolata Sulley, alisema katika hatua ya awali ya mapitio utafanyika utafiti kwa kupata maoni kutoka kwa wadau ili kuwa na sera bora inayozingatia haki na masuala ya kijinsia kwa watu wenye ulemavu.



# ... ACT Wazalendo yaweka msimamo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinaunga mkono uteuzi wa wajumbe wa makamishna wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) walioteuliwa hivi karibuni na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi. Akizungumza jana na Waandishi wa Habari, Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Salum Bimani, alisema wajumbe wa tume hiyo ni wanasheria wazoefu na wenye weledi katika masuala ya kuendesha uchaguzi na wana sifa zinazostahili.

Alisema wanawapongeza wateule hao kwa sababu wana uzoefu katika masuala ya kuendesha uchaguzi lakini amewatanabahisha kuwa wao ni watumishi wa wananchi wa Zanzibar na si wa mlengo wa itikadi ya kisiasa, hivyo wana wajibu wa kuangalia maslahi mapana ya Zanzibar.

Aliwataka kutumia vyema taaluma, weledi na uzoefu wao na kuwavusha wananchi katika hali ya shaka na wasiwasi kwa kutetereka amani kwa sababu ya uchaguzi.

"Tunapenda kuwatanabihisha makamishna hao kuwa wao ni watumishi wa wananchi na wasiwe wanachama wenye mlengo wowote wa kisiasa hivyo wanawajibu wa kuangalia maslahi mapana ya Zanzibar," alisema Bimani wakati akizungumza na waandishi katika ofisi za chama hicho, Vuga mjini Zanzibar.

Bimani alisema kwa Zanzibar uchaguzi ni biashara, uchumi, amani na mshikamano, hivyo akawataka wananchi kuwaunga mkono makamishna hao na kushirikiana nao kwa kuwapa kila aina ya msaada katika kutimiza majukumu yao. Pia alisema, ACT inaamini kuwa utendaji wenye uwadilifu wa tume hiyo utawezesha juhudi za kuleta mageuzi ya tume za uchaguzi katika mfumo wa uchaguzi, wa kidemokrasia kwa lengo la kuleta maridhiano endelevu.

"Tunaamini utendaji wenye uadilifu wa ZEC, utawezesha juhudi zinazoendelea za mazungumzo za kuleta mageuzi ya mfumo wa uchaguzi, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora wa kuleta maridhiano endelevu, amani na utulivu kuwa mwepesi kufikiwa na kuleta tija," alisema.

Hata hivyo, alisema chama hicho kimejiandaa vizuri kushiriki uchaguzi mdogo wa jimbo la Mtambwe utakaofanyika Oktoba, mwaka huu, baada ya aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo kufariki dunia na wana matumaini kushinda.

# Aweso awapa kibarua wakurugenzi maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema licha ya kuwapo mafanikio katika sekta ya maji bado baadhi ya maeneo yana changamoto hasa katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga kikao kazi cha wakurugenzi wa huduma kwa wateja wa mamlaka ya maji za Tanzania kilichofanyika visiwani Zanzibar.

Waziri alisema wanahitaji wakurugenzi wa huduma za maji ambao wako karibu na wateja wa maji ili muda wowote wanapokuwa na changamoto katika kupata huduma kutatua kwa haraka.

"Moyo wa mamlaka ya maji ni wakurugenzi wa huduma za maji, hivyo ni vyema viongozi kuwapa ushirikiano mzuri wakurugenzi hao," alisema.

Alisema ni vyema kuifanyia kazi changamoto ya utoaji wa huduma ya maji kwa sababu serikali imewekeza fedha nyingi katika sekta ya maji ili wananchi wapate huduma. Kwa hiyo, alisema mwananchi wanapaswa waunganishiwe maji katika muda mfupi.

Kwa mujibu wa Aweso, huo ndio umuhimu wa huduma kwa mteja huenda anaridhika, hivyo ni vyema utafiti ufanyike kuona wateja wanaridhika na huduma ya maji wanayopatiwa.

"Wakati mwingine eneo hili na uvujaji wa maji, unajisikiaje kujiita mkurugenzi wa huduma kwa wateja ilhali mwananchi hana maji? Unapita mtaani maji yanamwagika yanapotea wakati mamlaka ya maji ipo kwa ajili ya wananchi kupata maji na si kupotea," alisema. Pia alisema haiwezekani kuona maji yanamwagika na kupotea wakati gharama kubwa zinatumika kwa ajili ya uzalishaji wa huduma hiyo.

Waziri huyo alisema lazima kukubali teknolojia zitumike kufanya mageuzi katika sekta ya maji ili mwananchi aungiwe maji kwa njia ya teknolojia ili kupata huduma hiyo kwa haraka.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Joseph Kilangi, alisema bado Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) haijafikia hatua ya kujiendesha kulinganisha na mamlaka za maji Tanzania Bara.

Aliwataka watendaji hao kuendeleza kufanya kazi kwa bidii na uadilifu katika kutoa huduma ya maji ili kuiwezesha serikali kukusanya mapato yatokanayo na sekta hiyo kwa maendeleo ya nchi.




Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (kushoto) na Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Taifa Gas, Devis Deogratius wakifurahia jambo, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kutiliana saini makubaliano yatakayotoa fursa kwa benki hiyo kutoa mikopo ya mifumo ya gesi ya kupikia kwa taasisi mbalimbali zikiwemo shule, hospitali, magereza, viwanda, vyuo na watoa huduma za vyakula nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyama vyapinga uteuzi wajumbe ZEC

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya vyama vya siasa vimepinga muundo wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kwa madai kwamba ni uleule uliozoeleka ambao ulileta matatizo katika uchaguzi uliopita.

Kauli za wanasiasa wa vyama hivyo zimekuja baada ya Rais wa Zanzibar kutangaza uteuzi wa wajumbe wa tume hiyo ambayo Mwenyekiti wake ni Jaji George Joseph Kazi.

Mwenyekiti wa chama cha AAFP, Said Soud, alisema kabla ya muundo huo, vyama vya siasa vilipaswa kupewa taarifa na Rais ili kutoa majina mawili kwa vyama vya upinzani na majina hayo kujadiliwa na kukubaliwa kabla ya kutangazwa. Alisema, kwa mujibu wa taratibu za tume zinavyotakiwa kuwa haki na huru bado tume hiyo si haki na huru kwa sababu kama Rais ameteua tume watendaji hao watatekeleza matakwa yake.

Mwenyekiti huyo alisema iwapo itapatikana katiba mpya, tume hiyo haitopaswa kuwapo kwa sababu ili iwe huru haipaswi wajumbe wake kuteuliwa na Rais.


"Cha ajabu sisi kama chama cha siasa ambacho kimesajiliwa na tupo kisheria hatujapokea barua yoyote kuhusu muundo wa tume ya uchaguzi. Tunaona tu katika mitandao ya kijamii taarifa ya uteuzi wa wajumbe wa tume," alisema Soud.

Naye Hamad Masoud, Katibu Mkuu wa CUF, alisema uteuzi wa tume hiyo wameuona na kwa sasa Chama hakina maoni yoyote lakini mwenyekiti aliyeteuliwa ni mtu ambaye anajulikana msimamo wake ni kutoka CCM.

"Mwenyekiti huyo mpya namfahamu tokea akiwa Mrajis wa Mahakama na wakati ule wapinzani tunapeleka kesi mahakamani tunaona jinsi ya uendeshaji wa kesi," alisema.

Alisema CUF haipingi uteuzi huo lakini pia haishangazwi na uteuzi wa mwenyekiti huyo kwa sababu msimamo wake unajulikana. Kiongozi huyo alisema ili uchaguzi Zanzibar uwe huru na haki lazima katiba mpya ipatikane na kwamba mchakato wake umeshachukua muda mrefu.


Juzi, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alimtangaza Jaji George Joseph Kazi kuwa mwenyekiti mpya wa ZEC pamoja na wajumbe sita. Wajumbe hao ni Idrisa Haji Jecha, Juma Haji Ussi, Halima Mohamed Said, Ayoub Bakari Hamad na Awadhi Ali Said.



**RIHANNA**
UKURASA 14

Nipashe BT BURUDANI

JUMAMOSI AGOSTI 26, 2023



# WANACHAMBANA!

## Tatizo Diamond Platnumz

KUMECHAFUKA! Ndivyo hali ilivyo kwa wanamuziki wawili wa kike, Zuchu na Gigy Money ambao kwa sasa wapo kwenye vita kali ikiambatana vichambo na kutishiana kumwaga siri hadharani.

Mastaa hao wa Bongo Fleva, wamejikuta wakirushiana maneno makali kwa kile kinachodaiwa ni wivu wa kumgombea Diamond Platnumz.

Timbwili hilo lilianzia kwa mwanamtandao maarufu, Mange Kimambi ambaye aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram jinsi Diamond na Gigy Money walivyomzunguka Zuchu na kisha kukutana kimapenzi kwenye nyumba moja.

Inadaiwa tukio hilo lilitokea hivi karibuni wakati wasanii hao wote watatu walipokwenda kutumbuiza katika eneo moja maarufu kwa starehe jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Zuchu aliibuka na kukana jambo hilo huku akimtetea Diamond kuwa hawezi kujihusisha kimapenzi na Gigy Money kwa sababu sio aina ya wanawake anaowapenda.

Kauli hiyo ilionekana kumkera zaidi Gigy ambaye kwa kutumia akaunti yake ya Instagram, alimjia juu Zuchu na kutishia kutoa vitu vyao vya siri alivyonavyo vinavyomuhusisha yeye na Diamond kama njia ya kumziba mdomo.

Gigy akiwa na hasira amemtaja Zuchu kama mtu ambaye hajui lolote kuhusu yeye na Diamond wametoka wapi, alimkumbusha kwamba ana vitu vingi ambavyo yeye havijui.

Akaongezea kwamba kama kweli Diamond anampenda Zuchu, asingekataa kupanda gari moja wakati walikwenda eneo hilo la ufukweni, badala yake walipanda gari moja yeye Gigy na Zuchu, huku Diamond akipanda gari lingine.

"Kama kweli wewe (Zuchu) anakupenda wakati tunakwenda Kidimbwi ulimwambia Simba panda ndani ya gari, mbona bwana wako alikataa na akakuambia tupande gari moja mimi na wewe?" Alihoji

Kisha akaongeza "Kama anajiamini mbona hakutaka kukaa kati ya mimi na wewe, sasa uache kuniongelea hovyo iko siku utajuta," amesema Gigy Money.

Gigy ameongeza kwamba haogopi jambo lolote kwa sababu hana haja ya kugombea mwanaume kwa sababu maisha yake yanakwenda bila Diamond na kwamba anashangaa Zuchu kumsema vibaya na kumdhalilisha.

BASI SAWA

## Ukonga Wood waja 'Original'

KUNDI la muziki wa Hip hop linalojulikana kama Ukonga Wood, liameachia albam yao mpya yenye nyimbo 10 kali.

Akizungumza na BT, mmoja wa wasanii wa kundi hilo, Kabinova amesema albam hiyo inayoitwa Original, imeanza kupatikana katika majukwaa ya muziki ya mitandaoni.

Wasanii wengine wanaounda kundi hilo ni Shashow, G5 na Da Vanc Dinero.

Amesema nyimbo zote zimerekodiwa katika studio ya Black Dragon Music chini ya prodyuza yeye mwenyewe.

Kabinova amesema albam hiyo inaleta mapinduzi katika muziki wa Hip hop kibiashara na kuondoa dhana kwamba aina hiyo ya muziki haulipi.

"Muziki ni biashara kwa maana hiyo unatakiwa kukubali mapinduzi ili kukubalika katika majukwaa ya muziki," amesema.



## Patoranking kuitikisa Dar kesho

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Patoranking anatarajia kutoa burudani kabambe wakati atakapopanda jukwaani kuwaburudisha mashabiki wa jiji la Dar es salaam kesho.

Mkurugenzi wa Str8upvibes, Sniper Mantana amesema mashabiki wa muziki watakata kiu yao ya burudani kwa kucheza pamoja na mwanamuziki huyo nyota ambaye hivi karibuni atazindua albamu yake mpya inayoitwa WorldBest.

'Hii ni heshima kwa Tanzania na wadau kuona msanii kama Patoranking kuamua kuja kuimba nyimbo zake ya album yake katika nchi yetu, hayo yatafanyika katika chimbo la Kidimbwi Beach lililopo Mbezi," amesema





## RAYVANNY KAKOSA UVUMILIVU

MWIMBAJI na bosi wa lebo ya Next Level, Rayvanny ametoa kauli nzito kwa mashabiki wa muziki Afrika Mashariki ambao amewaelezea wana tabia ya dharau.

Msanii huyo alikuwa akizungumzia jinsi mashabiki walivyomdhihaki baada ya kuonekana kwenye tamasha lililojaa watu nchini Albania, na kuambiwa hana nguvu ya kujaza mashabiki kama vile na badala yake alialikwa.

"Msanii unafanya muziki ili uitwe? Sasa unaponiona mimi niko kwa shoo Albania unaanza kutafuta shoo si yake ni ya huyu, kama unaona ni rahisi kuitwa, uitwe wewe. Ukihitajika utaitwa kama unaona shoo ni rahisi..

Halafu kwenye shoo kama ya Albania unamuona Chui yuko pale, rangi nyeusi pekee na unapayuka," amesema Rayvanny.



## Harmonize amtolea macho Khaligraph

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, amemjia juu mwanamuziki wa Kenya Khaligraph Jones, baada ya kutoa maneno ya kuwaponda marapa wa Tanzania.

Katika moja ya ujumbe wa Jones katika mitandao ya kijamii, amesema hakuna rapa wa Tanzania anayeweza kushindana na yeye kwani mshindani wake mkubwa yuko nchini Nigeria.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Harmonize alimkaripia Khaligraph kwa kuonyesha dharau dhidi ya vipaji vya Kitanzania na kumuita mtu asiye na shukurani.

"Jinsi nilivyojitolea kwa bidii kukupa tuzo mwaka huu sikujua unaweza jihisi mkubwa hivyo na kuwadharau ndugu zangu.Unawajua Weusi, vipi kuhusu baba yako Profesa Jay? Kiwango chako sawa na Lunya na Con Boy county boy na bado wanakulalisha!! Ameandika.

## MONALISA USIUENDEKEZE MOYO

**Na Adam Fungamwango**

NIMEPITA kwenye mitandao ya kijamii nikakutana na meseji kibao za wasanii, mastaa na watu mbalimbali maarufu.

Nao pia baada ya shughuli zao wana maisha yao ya kawaida kama watu wengine. Wana furaha zao, changamoto mbalimbali kama binadamu wengine.

Mara nyingi baadhi ya watu huwakosoa wanapoposti maandishi yao kwenye mitandao ya kijamii, wakidai hawapaswi kwa sababu ni watu maarufu.

Hata wao pia wana haki ya kufurahia maisha, kuwa huru kufanya kitu chochote mradi tu havunji sheria.

Hapa nina meseji za mastaa wa kike ambao kila mmoja ameonyesha hisia zake na kutaka 'kushea' na watu kile alichokiandika kwenye mtandao wake wa instagram.

**Shamsa Ford**

Nguli wa sanaa na mcheza filamu wa kike, Shamsa Ford yeye aliandika maneno haya.

"Ni kweli unaweza kujilinganisha na wenzako, unaona kama umechelewa kwenye jambo fulani, lakini usisahau kuwa majira na nyakati za mafanikio zinatofautiana kwa kila mmoja wetu.

**Irene Uwoya**

Mwigizaji wa filamu na aliyewahi kushiriki mashindano ya ulimbwende 2006 na kushika namba tano, mwaka ambao Wema Sepetu alitwaa taji, Irene Uwoya, yeye akaandika hivi.

"Mungu nawaza watu wanavyotenda maovu, wanavyokudhihaki, wanavyotumia jina lako vibaya, kila kukicha ni mapya zaidi ya jana, tunavyokukosea kila leo. Ukiamua kushuka tutaweka wapi sura zetu? Mungu tuhurumie na uturehemu."

**Hamisa Mobetto**

Mwigizaji, mwimbaji na mfanyabiashara, Hamisa Mobeto yeye naye kwenye mtandao wake wa kijamii akachapisha maneno yafuatayo.

"Na pale unaposali siku hii ya leo.

Omba uwezo wa kuelewa kusudi lako. Mungu ameunda maisha yako kulingana na maelezo yako na kile anachojua ni bora kwako. Kamwe usichukie vikwazo kama kukataliwa, ni mabadiliko ya mahali unapohitaji kuwa. Jina lako liko katika sehemu ya juu zaidi."

**Matilda Sengo**

Mmoja wa waigizaji wanaovutia kuwatazama ni Maltida Sengo. Yeye naye kaja na hii.

Wakati mwingine unahitaji amani, kudeka, kuwa na mtu anayekusikiliza na kukuelewa, utajikuta ni mwenye furaha kuliko ulivyotegemea.

**Monalisa**

Ni mtunzi, mwandishi, mtayarishaji na mwongozaji wa filamu. Jina lake halisi ni Yvonne Cherrie, lakini ni maarufu kwa jina la Monalisa. Ameandika hivi.

"Maamuzi mengine yanahitaji akili na sio moyo au hisia zako. Kalagabaho."



FILAMU

# Chawa: Zaidi ya 'pro max'

**Na Adam Fungamwango**

SIKU hizi kuna neno maarufu sana la 'chawa'. Na ukisikia chawa siyo yule mdudu anayeng'ang'ania kwenye nywele au nguo za binadamu.

Chama hao wa siku hizi ni binadamu wenyewe kamili na si wadudu.

Tafsiri ya chawa wa sasa ni watu ambao kazi yao kumsifu, kumkweza na kumlinda mtu ambaye anawapa maisha.

Ni kwamba kuna baadhi ya watu maarufu wakiwemo wasanii siku hizi wanapenda sifa na 'kutrend', hivyo kuwatumia aina fulani ya watu wenye uwezo wa kumlinda, kumsifu na kumjibu yoyote ambaye atamgusa tajiri yao.

Kuna aina nyingi za uchawa, wengine kazi yao ni kumtafutia tajiri warembo tu.

Baada ya kutoa ufafanuzi kidogo juu ya neno chawa tutaiangalia filamu hii inayobeba jina hilo la chawa.

Imechezwa na Karim Kasambala, Vailet Frank, Halima Manyiri, Ngoma Nagwa, Kingwendu, Miss Buza, Layla Fakhi, Rahma Selemani, Boniface Matheo, Maulid Pembe na wengineo.

Kasambala ni kijana mwenye mke, lakini mvivu wa kufanya kazi. Hali hiyo inamletea matatizo na mkewe.

Mke anakwenda hadi kumtafutia mumewe kazi, lakini anaporudi anaambiwa alikwenda kutafuta mabwana.

Hatimaye mke anachoka na aina ya maisha ambayo mumewe anaamua kumkimbia.

Kasambala akili inamkaa sawa anaanza kutafuta vibarua. Lakini kutokana na kwamba hawezi kazi yoyote anaamua kuingia kwenye kazi ya uchawa.

Anakuwa kuwadi kwa wanaume wenzake na iliendelea mpaka siku moja alimuitia tajiri yake wanawake wawili ambao walikutana eneo moja.

Hii ilileta matafaruku na tajiri akaamua kumtimua. Yeye mwenyewe kwa sababu hana mke akawa anavamia wanawake ovyo kiasi cha kumtongoza mke wa jirani yake Malima.

Mke akaenda kumwambia mumewe akawa anatafutwa na mapanga.

Kazi ya uchawa ikaendelea, kuna tajiri mmoja yeye akataka amuuguze tu ndugu yake ambaye alikuwa na tatizo na mapafu na kifua. Pamoja na kwamba anapata matibabu kutoka kwa madaktari, lakini akataka awe mwangalizi wa karibu.

Kasambala anafanya hivyo hadi ndugu ya tajiri yake akapona. Kwa kile alichokifanya, tajiri huyo anampa nyumba nzuri na mpya.

Kijana huyo akamkumbuka mkewe, akaenda kumuomba msamaha na kumleta kwenye nyumba hiyo mpya.

Mwanamke haamini, lakini ukweli ndiyo huo, kazi ya uchawa ikawa imemlipa mumewe.





## Hongera Rihanna kampata mwana

MWANAMUZIKI nyota Rihanna (35) na mume wake A$AP Rocky (34) wamemkaribisha mtoto wao wa pili hivi karibuni.

Mtandao wa TMZ ulikuwa ya kwanza kuripoti habari za mtoto huyo, lakini wanasheria wa wanandoa hawakuweza kupatikana kwa maoni.

Rihanna alijiweka hadharani wakati ujauzito ukionekana dhahiri dakika za mwanzo za onyesho lake la Februari, pale msanii huyo alipoonekana akipapasa tumbo lake na kuacha.



## Yemi Alade pole yako

MWANAMUZIKI na mtunzi maarufu kutoka Nigeria Yemi Alade, ameibua mjadala baada ya kueleza amenusurika kifo kwenye ajali ya gari alipokuwa nchini Uhispania.

Katika chapisho lake kwenye Instagram siku ya Jumanne, msanii huyo amesema kwamba alipata ajali hiyo wakati alipokuwa akisafiri kati ya Barcelona na Benicassim.

Alisema ajali hiyo ilitokea ghafla lakini alitoka akiwa na majeraha madogo, na kupoteza ukucha pekee.

Alade, anayejulikana kwa muziki wake wa kusisimua, alisema licha ya ajali hiyo bado alitumbuiza jukwaani saa chache, kisha alikwenda kupata matibabu.

## Falz muombe Mungu utapona

RAPA na mwimbaji kutoka Nigeria, Folarin Falana, maarufu kama Falz The Bahdguy, ameelezea mateso anayoyapata kwenye goti ni makali.

Ripoti zinasema kwamba Falz alifanyiwa upasuaji wa goti Mei 2, 2023, katika kituo cha matibabu huko London, Uingereza.

Akitokea kwenye kipindi cha Cool FM, Falz amesema alifanyiwa upasuaji huo baada ya kuumia wakati akicheza soka.

"Ulikuwa wakati mgumu sana kwangu. Nilikuwa na upasuaji wa kujenga upya maungio yanayoshikilia goti. Kilichotokea ni kwamba kiungo hicho kilichanika kabisa na kunisababishia maumivu makali," amesema.





## Ron umewaacha wanakulilia

WASANII mbalimbali wamejitokeza kuomboleza kifo cha mkongwe wa majukwaa ya uigizaji, Ron Cephas Jones, kilichotokea mapema ya wiki hii

Mwigizaji huyo alijulikana zaidi kwa mfululizo wa filamu za This Is Us, alicheza kama baba aliyepotea kwa muda mrefu katika familia yake.

Jones alikuwa anasumbuliwa muda mrefu na matatizo ya mapafu, hayo ni kulingana na meneja wake.

Alipandikizwa mapafu mara mbili mnamo 2020, kulingana na ripoti za vyombo vya habari.

## Kanye haya tena umelikoroga

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West kwa mara nyingine amekuwa gumzo baada ya kulalamikiwa kuwa mpenzi wake hana maadili wakati wa ziara yao nchini Italia.

Katika ziara hiyo Kanye West na mke wake mpya, Bianca Censori, ilizua tafrani kwa wenyeji kutokana na mavazi yao kukosa heshima.

Censori alidaiwa kupigwa picha akiwa amevalia vazi fupi na lenye kubana ngozi hali iliyozua taharuki miongoni mwa wakazi wa kihafidhina wa nchi hiyo.

Kulingana na sheria ya Italia, mwana mama huyo anaweza kupewa adhabu kwa ukiukaji wa kanuni kwa kulipa faini ya dola 5,424.



HABARI KASKAZINI

# Polisi, bodaboda waisaidia shule mahitaji maalum

**Na Jaliwason Jasson,**
HANAN'G

JESHI la Polisi mkoani Manyara, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na waendesha pikipiki, maarufu kama bodaboda, wameikumbuka Shule ya Msingi Katesh A, yenye wanafunzi wa mahitaji maalum.

Wadau hao wametoa misaada ya kibinadamu ikiwamo vyakula kama mchele, sukari, mbuzi, maandazi, sharubati, mafuta ya alizeti, na mahitaji mengine ya sabuni, madaftari na kalamu.

Akizungumza jana, baada ya kukabidhi msaada huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, alisema wameona wasifanye tamasha la Polisi na bodaboda nyama choma festival na kula peke yao, bali waungane na wanafunzi wenye mahitaji maalum nao waweze kupata mahitaji.

Katabazi, alisema misaada hiyo imetolewa na waendesha pikipiki wa Katesh, kampuni ya Dutch Corner Limited na Mtandao wa Polisi wanawake Manyara.

Awali, Mwenyekiti wa waendesha pikipiki, maarufu bodaboda wa Wilaya ya Hanan'g, John Faustin, alisema waliamua kwenda kuwaona wakiwa na kilogramu 50 za mchele, kilogramu 25 za sukari, madaftari, kalamu na shalubati.

Alisema walifanya hivyo kwa kuwa baba akienda kwa mtoto ni lazima awe amebeba kitu au mtoto akienda kwa mzazi ni lazima awe amebeba zawadi.

Vilevile, mwakilishi wa kampuni ya Dutch corner limited Innocent Martin, alisema wao waliwaletea mchele kilogramu 100, sukari kilogramu 50, sabuni ya kufulia, mafuta ya Alizeti kwa ajili ya kupikia ili viweze kuwasaidia.

Martin, alisema kampuni yao huo ni mwanzo wataendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa jamii kwa kuwa ndio wateja wao.

Kwa upande wake mwalimu mkuu wa shule ya msingi Katesh A, Matilda Shao, aliwashukuru kwa sadaka hiyo waliyotoa kwa watoto.

Alisema hakuamini kama bodaboda wangeweza kushirikiana na polisi kwa kuwa huwa jamii inajua ni maadui ambao wanasababisha ajali na kukiuka sheria za barabarani.

Shao, alisema kwa mtu yeyote anayetoa msaada kwa watoto au kufanya kazi inayowahusu watoto ni lazima apate baraka nyingi na kila analofanya ni lazima lifanikiwe hivyo hawezi kupungukiwa na kitu.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kulia), akizungumza na wamiliki wa migodi na wachimbaji wa madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani juzi, kuhusu umuhimu wa kuchangia maendeleo ya jamii sehemu zinazowazunguka. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gration Makota. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vijiji vyaunda jumuiya uhifadhi Ziwa Natron

**Na Godfrey Mushi,**
LONGIDO

VIJIJI 39 vya tarafa za Longido, Ketumbeine na Engareibor katika wilaya ya Longido mkoani Arusha, vimeunda jumuiya mpya ya uhifadhi ya LOKEEN-NATRON, iliyojipa jukumu la kuhifadhi, kulinda na angalau kutumia rasilimali zilizoko kwenye ikolojia ya Ziwa Natron.

Akizungumza jana na wenyeviti wa serikali za vijiji hivyo na menejimenti ya Jumuiya ya LOKEEN-NATRON, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, alisema kuanzishwa kwa jumuiya hiyo, kutasaidia kuongeza nguvu ya kupambana na uvamizi katika ikolojia ya ziwa hilo.

Kabla ya kuifunda na kuionya jumuiya hiyo, alizindua majengo ya ofisi za jumuiya hiyo, kukabidhi kikosi cha doria chenye pikipiki nne, na gari maalum aina ya Toyota Land Cruiser. Jumuiya hiyo inafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la World Wildlife Fund (WWF) na UK Aid (From the British People).

'Mwezi Julai mwishoni, nilikuwa kule Magadini, nikawa nauliza hili Ziwa Natron mwisho wake ni wapi, wakaniambia zamani lilikuwa linafika Shule ya Msingi Magadini, lakini leo ukiangalia kutoka pale shuleni, mpaka lilipofikia ziwa ni kama kilomita nne au tano na linazidi kupungua zaidi. "Unapoyaona haya sio bahati mbaya. Msitu wa Longido, Msitu wa Gelailumbwa, na Msitu wa Ketumbeine, hali ni mbaya na imevamiwa. Kwenye misitu ile ndiko kwenye vyanzo vya maji vinavyohudumia maji wananchi wa Kata ya Noondoto, Namanga na Ilorienito, lakini na upande ule wa pili wa Kata ya Gelai Merugoi na Gelai Lumbwa.

"Kwa bahati mbaya sana, siku za karibuni misitu ile imevamiwa na wananchi, wengine wamejenga makazi, wengine wanalima kwenye msitu na wengine wameenda kulima mpaka kwenye vyanzo vya maji ndani ya mita 60.

"Sasa kama serikali hatuwezi kukubali hilo liweze kuendelea, wenyeviti wa vijiji wa maeneo hayo mpo na kwa sababu suala la mazingira ni la kisheria, hatuwezi kulifumbia macho na hatuwezi kukubali watu wachache waharibu vyanzo vya maji, wachache waingize ng'ombe kwenye vyanzo vya maji," alisema,

Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, Northern Tanzania), Prof. Noah Sitati, alisema mchakato wa kuanzisha LOKEEN-NATRON ulianza huko nyuma wakati akiwa na WMA mwaka 2015/16 lakini hawakuwahi kuisajili na baadaye tukakutana na hawa viongozi na kusema tunataka kuwa na chombo chetu kitakachotusaidia katika kazi za jamii.

"Tumeanza safari pamoja na tunapenda kuona kazi inaendelea vizuri, mlichaguliwa kuiongoza LOKEEN-NTARON, mna kazi kubwa sana, na mimi bila shaka niko nyuma yenu," alisema.

Mwenyekiti wa LOKEEN-NATRON, Peter Laitayok, alizishukuru WWF na UK Aid kwa ufadhili wao huku akisema wazo la kuanzishwa kwake liliasisiwa na Baraza la Madiwani la Wilaya ya Longido mwaka 2021.

"Ilikuwa wakati mwafaka kwa jamii ya Longido ya Lake Natron, kupata shirika mama la kusimamia maendeleo katika eneo lao. Eneo hili la liko bado ndani ya Pori Tengefu la Natron.

"Kwa hiyo hakuna jumuiya yeyote ya kijamii, ambayo ina jukumu la kuhifadhi, kulinda na angalau kutumia rasilimali. Kwa hiyo jamii imefaidika kwa kuona sasa wanayo rasilimali ya kutosha na wameanzisha shirika hili ili kushirikiana na wadau wengine kuleta maendeleo katika jamii ya Ziwa Natron," alisema.

# Waumwa sikio kurasimisha biashara za nje

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAFANYABIASHARA wanaouza mazao nje ya nchi kutoka Mkoa wa Arusha, wameng'atwa sikio na serikali wakishauriwa kurasimisha haraka biashara zao ili kuepuka kukutana na vikwazo wakati wa usafirishaji wa mazao hayo.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia ufuatiliaji wa menejimenti na ukaguzi, Ramadhan Madeleka, aliwasihi wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa hiyo badala ya kusubiri hasara wanayoweza kupata pindi mazao yao yanaposhikiliwa.

Alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku tatu, yalioandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

"Mafunzo haya yamekuja baada ya Agosti Mosi, mwaka huu, nyie wafanyabiashara kuomba mafunzo haya ili mpate uelewa wa usajili wa kampuni zenu kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, hivyo serikali imewapatia kwa gharama zake, hivyo naomba zingatieni elimu mtakayopata hapa ikalete tija zaidi kwenu na taifa,"alisema.

Aliwaomba wafanyabiashara hao kuhakikisha wanafuata taratibu zote za usajili na upataji leseni wa biashara zao ili zitambulike rasmi na kuepuka usumbufu wakati wa kazi zao.

Naye mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa BRELA katika mafunzo hayo mkoani Arusha, Isdor Nkindi, alisema mafunzo hayo wanayatoa kwa wafanyabiashara wa mazao nje ya nchi ili waelewe umuhimu wa kurasimisha biashara zao na kupata leseni ili wafanye kazi kwa uhuru. "Najua wenyewe walitoa ombi kwa serikali na serikali imesikiliza na leo inatoa mafunzo haya naamni baada ya hapa kila mmoja atafuata taratibu na kurasimisha biashara yake au kusajili kampuni yake ili kupata leseni itakayowezesha kufanya biashara hii bila kikwazo,"alisema.

Alisema anaamini mfanyabiashara siku zote anahitaji kuwa na mazingira rafiki, ili katika biashara zao wafanye bila kupata gharama kubwa na kupoteza muda, jambo ambalo serikali imejenga mazingira rafiki kwao kwajili ya kuwawezesha kufanya biashara bila mkwamo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Mao Chizma, alishukuru serikali kuwapatia mafunzo hayo yanayowajengea uelewa zaidi, katika usajili wa biashara zao na yamewasaidsia kuwaondolea woga waliokuwa nao.

"Awali tulikuwa tunaogopa kusajili biashara zetu tukidhani tutatozwa fedha nyingi serikalini, kumbe sivyo na hakuna usumbufu wowote. Sasa naamini tutasafirisha mazao yetu bila woga wala kutumia njia za panya, kwani tutapata leseni na kutusaidia kusafirisha mazao kiurahisi bila kikwazo,"alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

## VIJIJI VYA UJAMAA

# Pilika za kamatakamata Gezaulole, waliokubali leo wanaishi 'beach'

**Na Adam Fungamwango**



"SONGASONGA, Kimbiji, Tegeta na Mwanadilatu, hayo ndiyo hasa makao ya mwana wa mapinduzi...Gezaulole baba, Gezaulole mama eee, biashara ya njugu na korosho sasa haitufai eee."

Leo nimeanza na wimbo uliovuma sana katikati ya miaka ya 1970 uliopigwa na bendi ya Urafiki Jazz, iliyokuwa inamilikiwa na Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kilichopo maeneo ya Ubungo jijini Dar es Salaam.

Ulikuwa ni utunzi wake kiongozi wa bendi hiyo, marehemu Juma Mrisho, maarufu kama 'Ngulimba wa Ngulimba, wimbo uliitwa 'Gezaulole.'

Nimeanzia hapo ili kuonyesha maeneo ambayo kwa sasa ndugu yangu kupata kiwanja ni mtihani wa aina yake.

Inabidi uwe na pesa nyingi ili uweze kupata kiwanja kwani baadhi ni maeneo ambayo ni ufukweni mwa bahari, hasa huko Geuzaulole.

Miaka ya 1970 maeneo hayo yalikuwa ni mapori tu. Narudia tena, siyo vijiji ila ni mapori.

Watu wasiokuwa na kazi maalum mijini walikuwa wanakamatwa na kupelekwa kwenye mapori hayo ili wakaishi huko na msingi mkubwa ikiwa ni kupatiwa ardhi bure ili walime.

Msingi wa yote hii ilitokana na sera ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipoanzisha sera ya Ujamaa, na kuchapisha mwongozo ulioitwa 'Azimio la Arusha', ili kuondokana na sera ya ubepari.



Katika mwendelezo wa hilo, mwaka 1972 alianzisha Vijiji vya Ujamaa katika mikoa yote ya Tanzania.

Kwenye makala hii nitajikita zaidi kwenye jiji la Dar es Salaam ambalo liliitwa Mzizima ambapo kulikuwa na mapori pamoja na vijiji vidogo kama ambavyo bendi ya Urafiki imeviainisha kwenye wimbo wao ambavyo ni 'Kibugumo', 'Kimbiji', 'Mwanadilato' na 'Gezaulole', 'Tegeta', Kunduchi,' 'Mbezi Beach' na maeneo mengine kama Boko ambako kulikuwa na mapori tu.

Lengo kubwa la Nyerere pamoja na serikali yake ilikuwa ni kuwataka vijana waachane na biashara za umachinga, uchuuzi, kama vile kuuza karanga, korosho, maji ya baridi, na kujikita kwenye kilimo cha pamoja chenye tija.

Siyo mikoani tu ambako kulikuwa na mapori, hata Dar es Salaam wakati huo ilikuwa haijapanuka sana na maeneo waliokuwa wanaishi zaidi watu ni Ilala, Kinondoni, Manzese na Magomeni. Sehemu kubwa iliyobaki hata Mwananyamala, Kigogo, Mburahati, bado kulikuwa hakujachangamka sana ingawa watu waliishi.

Watu walihimizwa kutoka mijini kwenda vijijini kulima, na maeneo yalikuwa yakitolewa bure na serikali.

Lakini baadhi ya watu walikuwa wabishi hawakuta kwenda. Nani angependa kutoka mjini na kwenda kuishi vijijini au porini? Walipiga chenga. Serikali ikabidi ianze kutumia nguvu kwa kuanza kamatakamata.

Hata waliokamatwa kwa nguvu kupelekwa, walikaa muda mfupi baadhi yao wakatoroka tena kurudi mjini.

Wakosoaji walidai ilitumika nguvu kubwa kuwapeleka watu vijijini na maporini bila kuanza kutoa elimu kwa wahusika kwenye operesheni hiyo ya Vijiji vya Ujamaa.

Wakadai watu walitolewa kwenye makazi yao ya asili na kupelekwa maporini, ikidaiwa baadhi walikufa kwa kushindwa kumudu mazingira, kuuawa na wanyama kama simba, chui, pamoja na ugonjwa wa malaria.

Hata hivyo, Nyerere na serikali yake ilikuwa na maono ya mbali sana kwani leo hii hao hao waliokuwa waking'ang'ania kukaa Manzese, Ilala na kukataa kwenda Kunduchi, Gezaulole, Goba na kupewa ardhi ya bure wanajuta.



Ujanja wao wa wakati huo leo ni mauti na umasikini.

Leo walioonekana wajinga na kukaa kuvumilia tabu zote wakimiliki ardhi waliyopewa bure na serikali leo wao au familia zao zinaishi maisha mazuri. Wanakaa sehemu nzuri kwani kwa sasa si vijiji au mapori tena bali ni maeneo ya 'ushuani.'

Ardhi yake ina thamani kubwa kwa sasa. Walioonekana wajinga wakati huo kwa sasa wamejenga majumba maeneo hayo ghali, wameingia ubia na matajiri au kuuza viwanja na kujipatia pesa nyingi ambazo zimewafanya kujenga majumba ya kifahari kwa sasa maeneo mengine na kuendesha biashara zao. Kama siyo wao, basi watoto wao au wajukuu wamenufaika.

Kama ingewezekana kurudisha miaka nyuma, halafu leo ikatokea wito kama huo, nadhani wala isingetumika kamata kamata, wananchi wenyewe wangekimbilia vijijini na maporini. Wangejua kuwa baada ya zaidi ya 10 maeneo hayo yangekuwa ghali na kusingekuwa tena porini, kungejengeka kama inavyoonekana hivi sasa.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Matokeo uchaguzi mkuu Zimbabwe yaanza kutolewa

**HARARE,** ZIMBABWE

MATOKEO ya awali kutoka kwenye majimbo yameanza kutolewa baada ya wananchi wa Zimbabwe kupiga kura katika uchaguzi mkuu uliofanyika majuzi.

Matokeo hayo yalianza kutolewa juzi kutoka katika kata mbalimbali baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika kwa baadhi ya vituo.

Hata hivyo, kuna malalamiko kutokana na baadhi ya wanaharakati wa mashirika ya kiraia kukamatwa na polisi.

Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnagangwa, alishiriki zoezi la kupiga kura Jumatano, huku wafuasi wake wengi wakitarajia kufanyika mabadiliko baada ya miaka mingi ya hali ngumu ya kiuchumi. Baadhi ya wachambuzi walieleza kwamba, kuna uwezekano mdogo wa chama tawala cha ZANU-PF kuachia madaraka baada ya kutawala nchi hiyo kwa miaka 43.

Katika matokeo hayo majimbo 10 kati ya 210 yalikuwa tayari yametangaza matokeo yake.

Hata hivyo, ni mapema kutabiri muelekeo wa hali itakavyokuwa na chama gani kitabeba viti vingi vya bunge na madiwani.

Juzi muda wa upigaji kura uliongezwa kwa kata 40, inatokana na ukubwa wa vitongoji vinavyowakilisha chini ya asilimia 1 ya kata zote 12, 274.

Tume ya uchaguzi imefafanua kuwa, kuongezwa kwa muda huo kumetokana na kuchelewa kwa uchapishaji wa karatasi za kupigia kura.

Rais Mnangagwa (80) alichukua nafasi hiyo kutoka kwa Robert Mugabe baada ya mapinduzi ya mwaka 2017 na baadaye kushinda uchaguzi wa 2018.

Mpinzani wake mkuu kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu uliopita, Nelson Chamisa, kutoka chama cha CCC anachuana vikali na Rais Mnangagwa.

Promose Mkwananzi, msemaji wa muungano wa upinzani wa CCC alisema kwamba wanahisi mchakato wa uchaguzi una dosari nyingi na hauwezi kutoa matokeo sahihi. Hata hivyo, walifahamu hilo mapema, na ndio maana wamejitayarisha kushinda uchaguzi usio huru na haki.

Marekani imeishtumu mamlaka ya Zimbabwe kwa kuhujumu zoezi zima la uchaguzi kwa kuwakamata waangalizi wa uchaguzi kutoka Marekani na kuitaka serikali kuwaachia huru.

Msemaji wa wizara ya mambo ya nje wa Marekani Mathew Miller ameandika kwenye mtandao wa kijamii wa X, kwamba uvamizi huo wa polisi dhidi ya mashirika ya kiraia yanayoangalia uchaguzi , unaonyesha wazi kuwa serikali ya Zimbabwe haiheshimu uchaguzi huru na wa haki.

Polisi ilisema imewakamata waangalizi 41 wa uchaguzi, na kuchukua tanakilishi na simu zao za rununu.

Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), limesema kuwa serikali inakwenda kinyume na ahadi yake ya kuruhusu uangalizi wa uchaguzi.

**DW**

## Trump ajisalimisha gerezani

**GEORGIA,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump amejisalimisha katika gereza moja la Georgia, kabla ya kuachiwa huru kwa dhamana.

Trump anatuhumiwa kupanga njama ya kutengua matokeo ya uchaguzi wa jimbo hilo mnamo 2020 na kutakiwa kukamatwa.

Kiongozi huyo alilazimika kulipa bondi ya dhamana ya dola 200,000 kama dhamana.

Baada ya kutoka mahakamani, alielezea kesi hiyo kama ukiukaji wa haki.

Ni mara yake ya nne kukamatwa katika kipindi cha miezi mitano akihusishwa na kesi ya jinai, lakini jana ilikuwa mara ya kwanza kupigwa picha akiwa na polisi.

Trump baadaye aliweka ujumbe wa kwanza katika ukurasa wake wa X, akielezea hatua hiyo ni sawa na uingiliaji wa uchaguzi.

Kiongozi huyo wa zamani anajiunga na orodha ya watu mashuhuri wa Marekani ambao wamewahi kukamatwa, ikiwa ni pamoja na Elvis, Frank Sinatra, Al Capone na Dk Martin Luther King Jr.

**BBC**



Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump akizungukwa na polisi baada ya kujisalimisha katika gereza la Geogia nchini Marekani jana. **PICHA: AFP**

# Rais Putin agusia kifo cha Prigozhin

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin amevunja ukimya baada ya kuzungumzia kuhusu ajali ya ndege iliyomuua kiongozi wa kundi binafsi la kijeshi la Wagner, Yevgeny Prigozhin.

Putin alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, lakini hakuzungumzia moja kwa moja kuhusu kifo hicho kilichosababishwa na ndege aliyokuwa akisafiria kuanguka kwenye mji wa Tver nchini Russia.

Katika ujumbe alioutoa kwa njia ya video, alimuelezea Prigozhin kama kiongozi aliyekuwa na kipaji, aliyefanya makosa makubwa katika maisha yake lakini pia aliyefanikiwa kuleta matokeo yaliyohitajika.

Wachambuzi wanasema ni vigumu kubaini iwapo kiongozi huyo wa wagner ameuawa au la.

Taasisi ya Serikali ya Russia inayohusika na masuala ya usafiri wa anga ilisema Prigozhin, pamoja na kamanda wa ngazi ya juu Dmitri Utkin, ni miongoni mwa watu 10 waliokuwepo katika ndege hiyo iliyopata ajali siku ya Jumatano.

Taasisi hiyo ilisema hakuna mtu aliyenusurika katika ajali hiyo.

Wakati huo huo, Russia ilisema Ukraine imerusha kombora kuelekea mji mkuu wa Moscow na kuishambulia Crimea kwa idadi ya ndege 42 zisizokuwa na rubani. Russia ilitaja tukio hili kuwa moja ya mashambulio mabaya ya angani yaliyoratibiwa na Ukraine dhidi yake.

Wizara ya ulinzi ya nchi hiyo, ilisema makombora aina ya S-200 yaliyovurumishwa katika eneo la Kaluga linalopakana na mji wa Moscow, yalidunguliwa kupitia mifumo ya ulinzi wa anga.

Gavana wa Kaluga Vladislav Shapsha, alisema hakuna mtu yeyote aliyejeruhiwa katika tukio hilo. Wizara hiyo ilisema pia kwamba Crimea, ambayo Russia iliinyakua kutoka Ukraine mwaka 2014 ilishambuliwa. Ndege 9 zisizokuwa na rubani zilidunguliwa kupitia mifumo ya ulinzi wa anga na nyingine 33 zilidunguliwa kabla ya kufikia malengo yake baada ya kuzuiwa na mitambo ya kielektroniki.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NOEL JOSEPH SHANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya RAV 4 yenye usajili namba T 313 AYY. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/696/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**WITNESS P LYIMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4970/0192/2019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MURIET SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA**:
**ARU/ARU/MUR/RB/235996/2023**

## KUPOTELEWA NA HATI YA NYUMBA

Ndugu **SALVATORY LUGAKINGILA BANYENZA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya nyumba, ya **Plot No. 75 "AA"** Hamugembe Manispaa ya Bukoba. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/239758/2023,** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0678564384**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**ABDULSAMAD MUFFAZAL ESSAJEE** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 187005** iliyotolewa makao makuu **DAR ES SALAAM PCO** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/4495/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 89/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ANNA THIMOTHY MASSAWE wa BIGWA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JUMA RAMADHANI KALABAKA**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **30** Mwezi **08** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 18 m wezi 08 mwaka 2023

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 76 YA MWAKA 2022**
**PILI HAMAD KAJULA ............MDAI**
**VERSUS**
**JUMA POLEPOLE KAJULA ............MDAIWA 1**
**THOBIAS AMON JACKSON ............MDAIWA 2**
**TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC.........MDAIWA 3**

**KWA: THOBIAS AMON JACKSON**

**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 31.08. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 ya mwezi wa AGOSTI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya UVINZA**
**Kituo cha NGURUKA**
**Mkoa wa KIGOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 4/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PILI IDDY MKOWA wa NGURUKA KATI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUWATEUA WASIMAMIZI YALIYOLETWA NA MUSA HEMEDI HASHILY PAMOJA NA IDDY RAMADHANI BARAKA**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **08** Mwezi **09** mwaka **2023** kabla hao waombaji hawateuliwa kuwa wasimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 08 mwaka 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA IRINGA MJINI**
**WILAYA YA IRINGA**
**TALAKA NAMBA 29/2023**

**INNOCHENSIA BATISTA MWINUKA MDAIDHIDI YA THOMAS ROMANUS MDAIWA MAOMBI YA TALAKA** Unatakiwa kufika mahakamani tarehe 13/09/2023 saa 2:30 kwajili ya shauri la talaka usipofika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25/08/2023.

**HAKIM MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO
IRINGA MJINI

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-23

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Mpelelezi yeyote huangalia mauaji yamefanyika vipi na hapo anaweza kuanza kudhani au kuhisi muuaji anaweza kuwa nani.

Aina ya nne ya mauaji ni kwamba wauaji ni kama hawana roho wala hisia, unaweza kusema wenye matatizo ya akili. Huua taratibu na kwa mateso makubwa mno. Hawa ndio wale hutenganisha viungo kimoja baada ya kingine na wakati mwingine kujirekodi wakati wanafanya hivyo.

Aina ya tano ni wauaji wenye msongo wa mawazo, hufikia kuona kila mmoja ni adui yake hivyo huchukua silaha na kutafuta kadamnasi ya watu na kuwafyatulia risasi, na mara nyingi huishia na kujimaliza na risasi ya mwisho.

Huu ndiyo msingi alioanza nao Eddy. Alijua kabisa muuaji alibebwa mno na hisia, inawezekana ikawa za mapenzi, ndiyo maana alimuua na kukatakata viungo, au kukatakata viungo kabla ya kumuua.

Ni mtu anayekupenda zaidi na baadaye kutokea kukuchukia zaidi ndiyo hufanya hivyo hivyo kwa sababu ya hisia. Ni mapenzi ndiyo husababisha mauaji ya aina hiyo.


Ndiyo maana Eddy alishughulika zaidi kufuatilia nyendo za Charton Antony. Na ikawa kama anavyohisi. Mpaka sasa ni yeye tu ndiye aliyekuwa anajua. Hata mjomba wa Tessy hakujua chochote.

Familia yote ilifahamu kuwa wakati mwili wa Tessy unaokotwa Kinondoni Msufini mumewe Charton alikuwa Dodoma kikazi.

Tayari Eddy Kamal alishakamilisha kazi yake ya kumfahamu muuaji. Muuaji wa Tessy ni mumewe Charton. Kilichobaki ambacho alichotaka kufanya ni kwa nini alimuua?

Alijua ni mapenzi kwa sababu ya kitendo cha kumkodisha Patauli anayeonekana ni jambazi, aliyekuwa akimsaidia kumtesa na kukatakata viungo vya mkewe.

Je Chatron alisikia nini mpaka kutengeneza mipango ya kumuua mkewe ambayo alionekana alipanga taratibu, kwa muda mrefu, huku akijitahidi kutoacha alama na ushahidi wa hata kuhisiwa? Kabla ya kumtia mbaroni Charton hii ndiyo kazi iliyobaki ya kukusanya ushahidi wote ili kukamilisha operesheni aliyo nayo ya mauaji ya Tessy ambayo awali watuhumiwa wake walikuwa ni waokota makopo na wazoa taka mitaa ya Kinondoni Msufini kwa sababu tu kiroba cha maiti kilikutwa maeneo hayo.




**"Una namba zao wote wawili?" Eddy akauliza.**

==============================

Tinga Patauli naye alikamatwa. Awali alikataa katakata. Eddy alijua hivyo. Haiwezekani mtu mwenye roho mbaya kama huyo akubali kirahisi.

Mtu ambaye kazi yake ni kukatakata viungo vya binadamu mwenzake awe na roho nyepesi ya kukubali kirahisi akiri anayoyafanya.

Kifupi Patauli ni jambazi sugu. Tena wale ambao kazi yao ni kuua kwa mateso. Siyo kama wale wadunguaji ambao kazi yao ni kumtafuta au kumfuata mhalifu na kuachia risasi moja au mbili, halafu anaondoka.

Huyu yeye anakaa na mtekwaji ana kwa ana, akimuuliza maswali ya kizushi, akimdhihaki huku akikata kiungo kimoja baada ya kingine.

Watu maalum kwa kazi hiyo walimnyong'onyesha na hatimaye akakiri kufanya hayo, huku pia akionyesha baadhi ya ushahidi wa vitu mbalimbali vilivyotumika kumuua Tessy.

Leo yupo mbele ya Eddy. Alitaka kufahamu machache kuhusiana na mauaji hayo. Akasema yeye alikodiwa na Charton kwa kazi hiyo kwa sababu peke yake asingeweza kuifanya.

Akasema Charton alikuwa amekereka baada ya kugundua kuwa mkewe ana mahusiano na mwanaume mmoja ambaye hata hivyo alitafutwa na hajaonekana.

"Kusema kweli kabla ya kumuua Tessy, mtu wa kwanza kuuawa angekuwa ni huyo mwanaume."

"Alikwambia anaitwa nani?"

"Barton."

"Yeye Charton alishawahi kumuona huyo Barton?"

"Hilo sina uhakika. Unajua mimi niliitwa kwa kazi hiyo ya kumtesa na kumuua Tessy, mengine sikuwa namuuliza sana kwa sasbabu kitu hicho kilionekana kumuumiza sana. Jamaa ana hasira na wivu sana kwa mkewe."

"Mlimtafuta kwa siku ngapi Barton?"

"Mmh! Ulikuwa ni msako wa hatari, unajua jamaa ana pesa, halafu anafanya kazi serikalini, hivyo jamaa alisakwa kama mhaini lakini hakupatikana. Baadaye taarifa zikaja kuwa huenda alijiua, wengine wakasema baada ya kusikia hivyo akatoroka nchi."

"Unamfahamu rafiki yake yeyote wa kike?"

"Nawafahamu wawili, Nancy na Rukia. Nancy ni mpenzi wake wa muda mrefu, lakini huyu Rukia ni wa hivi karibuni kama miezi minane tu iliyopita."

"Una namba zao wote wawili?" Eddy akauliza.

"Ndiyo."

"Naziomba."

Pamoja na kujua kila kitu bado kuna kitu ambacho kilimfanya asimalize kazi kwa kumkamata Charton.

Ilionekana kuwa kazi imekamilika. Tessy ameuawa na mumewe Charton kwa sababu ya wivu wa mapenzi. Na mwanaume ambaye anadaiwa kuwa naye ni Barton ambaye mpaka sasa hajulikani alipo.

Angeweza kumwambia Inspekta Frank atangaze rasmi kuwa muuaji au wauaji wa Tessy wamepatikana. Ni watu wawili akiwemo mumewe Charton. Lakini hakutaka kufanya haraka kiasi hicho.

Eddy anaomba namba za wapenzi wa Charton. Nia yake hasa ni nini?

"Enhee, mlipochukua mzigo wa maiti na kumbebesha Mboneka Fisimaji mliupeleke wapi?"

"Tulienda nao mpaka Magomeni Makumi. Pale tulichofanya ni kubadilisha gari tu kwa sababu za kiusalama. Tulimuacha Mboneka na yule dereva taxi waondoke, tukakodisha gari nyingine mpaka Kinondoni."

"Halafu?" Akauliza Eddy.

"Ilikuwa ni Kinondoni Biafra, tulipofika pale tuliwakuta vijana fulani wahuni. Tukawaita na kuwapa mzigo tukawaambia wakatupe popote pale na tukawalipa pesa. Wao sasa ndiyo wakawa wanajua wenyewe wapi waliupeleka."

Eddy ndipo alipofahamu kwa nini mabaki ya viungo vya Tessy yalionekana kwenye kiroba maeneo ya Kinondoni Msufuni.

Ni kwamba Tessy aliuawa Ukonga Banana. Maiti ikafungwa kama mali au mzigo kutoka huko mpaka Magomeni Mikumi. Halafu watu wakakodi tena gari hadi Kinondoni Biafra.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NAMUNGO YANASA BEKI WA NKANA FC

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU Ya Namungo FC imefanikiwa kumsajili beki wa kati mpya kutoka Nkana Red Devil FC ya Zambia, Derick Mukombozi, kwa kumpa mkataba wa mwaka mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba, alisema taratibu zote za usajili wa mchezaji huyo zimekamilika na wanaamini atakisaidia kikosi chao.

**Mkadeba alisema mchezaji huyo amesajiliwa kwa kufuata mapendekezo ya Kocha Mkuu, Cedrick Kaze, ambaye aliridhishwa na ubora wake.**

"Derick atasaini mkataba huo leo (jana) jioni, tunaamini ataleta ushindani ndani ya timu yetu kwa sababu ana uwezo mkubwa, usajili huu utaleta mafanikio katika kikosi chetu," alisema Mkadeba.

Aliongeza anaamini katika mapumziko yaliyopatikana benchi la ufundi litaendelea kufanyia kazi mapungufu na timu itarejea ikiwa imara kuendelea kusaka pointi muhimu.






Wachezaji wa soka vijana kutoka sehemu mbalimbali jijini wakifanya mazoezi ya kujiimarisha kwenye Uwanja wa JMK Park, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kipanga yasajili wapya nane*

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAKATI imeamua kuweka kambi Dar es Salaam, kikosi cha Kipanga kimesajili wachezaji wapya nane kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar inayotarajiwa kufanyika kuanzia mapema mwezi ujao, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Hassan Abdulrahman, alisema kilichowasukuma kuweka kambi ya mapema ni kuhakikisha wachezaji wanaimarika na kuwa tayari kupambana.

Abdulrahman alisema wanataka kuona kikosi chao kinamaliza katika nafasi ya juu tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita. Kocha huyo alisema msimu uliopita ulikuwa mbaya kwao ingawa walinusurika kushuka daraja baada ya kushinda michezo yao miwili ya mwisho na hivyo hawataki hali hiyo ijirudie.

"Tumeongeza nguvu katika kikosi chetu kuelekea msimu mpya, wachezaji wapya wako nane na tumewasajili kutoka timu za Tanzania Bara na wengine hapa hapa Zanzibar, watatusaidia kufikia malengo," alisema kocha huyo.

Alitaja nafasi ambazo wamezipa kipaumbele katika usajili wao ni ya ushambuliaji, kipa na mabeki baada ya kuwa na changamoto kubwa msimu uliopita.

"Tumesajili wachezaji wazoefu watakaoipa timu matokeo bora, tumejipanga kufanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, tunataka kuwa bora zaidi ikilinganishwa na msimu uliopita ambao upepo mbaya uliikumba timu yetu,"Abdulrahman alisema.

## Singida yatua Dar kwa mkwara, kuivaa JKU Shirikisho Afrika

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Singida Big Stars kimetua jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya mechi ya mkondo wa pili wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya JKU ya Zanzibar unatakaochezwa kesho Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kikitamba kuibuka na ushindi mnono na kwenda kukutana na Future ya Misri, mechi ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo Hussein Massanza, amesema wamewasili Dar baada ya kucheza mechi yao ya Ligi Kuu dhidi ya Prisons Jumanne iliyopita na kutoka suluhu kwenye Uwanja wa Liti, Singida, akibainisha kuwa wachezaji wao wote wako fiti kwa ajili ya mechi hiyo ambayo watakuwa ugenini.

"Tupo Dar es Salaam tayari, tumewasili jana (juzi) kwa ajili ya mechi hiyo, najua itakuwa ngumu kwa sababu mpira siku zote una matokeo katili na ya ajabu, lakini kwa hali ya kawaida tu ni kwamba tuna matumaini makubwa ya kusonga mbele na kwenda kukutana na Future ya Misri," alisema Massanza.

Massanza aliwaonya JKU wasijidangaye kudhani wanaweza kushinda mabao 3-0 kiurahisi kwani wamejipanga kwa kila njia kuhakikisha wanalinda ushindi wao wa mabao 4-1 walioupata awali.

Ijumaa iliyopita Singida Big Stars ilishinda idadi hiyo ya mabao kwenye uwanja huo huo ambao washindi walikuwa nyumbani.

JKU nayo itautumia uwanja huo kama uwanja wake wa nyumbani na mshindi wa jumla atakwenda kucheza raundi ya kwanza dhidi ya Future ya Misri, Septemba 15 nyumbani, kabla ya kwenda kukabiliana nayo ugenini mechi ya mkondo wa pili, Septemba 29.

## Katwila : Ihefu SC yaipania Mashujaa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila, amesema kikosi chake kitaendelea kufanya mazoezi ya nguvu katika kipindi cha siku 20 ambacho Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kwa ajili ya kupisha kalenda ya kimataifa.

Ihefu FC ilianza msimu mpya kwa kufungwa na Geita Gold FC na mechi yake ya pili ikapata ushindi wa bao 1-0 mbele ya Kagera Sugar, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Highland Estate, Mbarali.

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema lengo la kutosimamisha mazoezi ni kujiandaa na ushindani mkubwa uliopo na anataka kuona kikosi chake kinapata matokeo chanya katika kila mechi.

"Hii ligi msimu huu ina tofauti kubwa na msimu uliopita, ukiangalia timu zote zimejipanga vizuri na kila mtu anahitaji kufanya vizuri, tunahitaji kujiweka sawa kwa kufanya maandalizi mazuri kabla ya ligi kurejea kwa mara nyingine," Katwila alisema.

Aliongeza anafahamu mechi inayofuata dhidi ya Mashujaa FC ya Kigoma haitakuwa rahisi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAZARD ATAKIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inapanga kusajili mchezaji huru raia wa Ubelgiji, Eden Hazard, kwa kumpa mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea na Real Madrid mwenye umri wa miaka 32, mkataba wa mwaka mmoja. (***Football TransferS***)

### TONEY AGOMBEWA ENGLAND

KLABU ya Brentford imeweka bei ya pauni milioni 80 kwa mshambuliaji wa England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 27, huku Arsenal na Tottenham Hotspur zikiwa na nia ya kumsajili mchezaji huyo Januari. (***tIMES***)

### TIERNEY KUTUA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kufikia makubaliano na Real Sociedad kuhusu usajili wa mkopo wa msimu mzima kwa beki, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 26. (***The Athletic***)

### ARSENAL, MONACO SAFI

ARSENAL imeafikiana na Monaco kwa ada ya euro milioni 45 pamoja na nyongeza kwa mauzo ya mshambuliaji wa Marekani, Folarin Balogun, mwenye umri wa miaka 22. (***RMC Sport***)

### EVANS, UNITED KITAELEWEKA

KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano ya mkataba wa mwaka mmoja na Jonny Evans, mwenye umri wa miaka 35 katika hatua ambayo inaweza kuibua shaka juu ya mustakabali wa beki mwenzake, Harry Maguire (30) pale Old Trafford. (***Telegraph***)

### MASON KUELEKEA ALBANIA

KLABU ya Albania ambayo haikutajwa jina imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 21 baada mchezaji huyo na United kufikia uamuzi wa kuondoka Old Trafford. (***Talksport***)

### SPURS YAMBANIA JOHNSON

TOTTENHAM Hotspur inavutana na Nottingham Forest kuhusu ada ya kumsajili, Brennan Johnson, huku klabu hiyo ya East Midlands ikionyesha haiko tayari kumruhusu mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuondoka kwa kitita cha pauni milioni 40. (***Standard***)

### JOHNSON ATAJWA CHELSEA

CHELSEA imeonyesha nia ya kumsajili, Brennan Johnson (22) na mchezaji huyo anafikiriwa sana kujiunga na klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Stamford Bridge. (***Football London***)

### CITY YAMKOMALIA NUNES

KLABU ya Manchester City inajiandaa kuwasilisha ofa ya pili kwa Wolves ili kumnunua kiungo wa kati wa Ureno, Matheus Nunes, mwenye umri wa miaka 24 baada ya dau la kwanza la takriban pauni milioni 47 kukataliwa. (***Telegraph***)

### CANCELO KUTUA BARCA

BARCELONA itamsajili Joao Cancelo kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Manchester City siku chache zijazo, lakini hakutakuwa na chaguo la kumnunua beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 29. (***Marca***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL: SALAH HAWEZI KUONDOKA

**Klabu hiyo inajipanga kukata ofa nono kutoka kwa Waarabu...**

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL itakataa ofa yoyote ya Mohamed Salah, vyanzo vimeiambia ESPN, baada ya majaribio ya mabingwa wa Saudi Arabia, Al Ittihad kumfanya mshambuliaji huyo kuwa mchezaji wanayemwinda zaidi.

**Salah mwenye umri wa miaka 31 ameonekana kulengwa na Al Ittihad, ambao wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri kuunda ushirikiano na mshabuliaji wa zamani wa Real Madrid, Karim Benzema katika timu hiyo yenye maskani yake katika jiji la Jeddah.**

Fabinho, mchezaji mwenzake wa zamani wa Liverpool, aliondoka na kwenda Al Ittihad kwa ada ya pauni milioni 40 mwezi uliopita, vyanzo vimeiambia ESPN klabu hiyo ya Saudi iko tayari kulipa ada kubwa na mshahara mnono ili kumsajili Salah, ambaye alisaini mkataba mpya wa miaka mitatu pale Anfield mwaka jana.

Lakini licha ya uwezekano wa Liverpool kumwekea Salah ada kubwa kwa kumruhusu mchezaji huyo kuondoka, vyanzo vimesema klabu hiyo haina nia ya kuachana na nyota huyo.

Liverpool inafahamu nia ya Al Ittihad, lakini bado haijapokea ofa yoyote rasmi au isiyo rasmi kutoka kwa klabu hiyo, lakini ofa kwa Salah itakataliwa.

Ingawa dirisha la usajili la majira ya joto linafungwa Septemba Mosi, dirisha la uhamisho la Saudia limesalia wazi hadi Septemba 20, na kuziwezesha timu zake kusajili wachezaji kutoka Ulaya kwa wiki tatu zaidi baada ya dirisha lao la biashara kufungwa.

Mapema mwezi huu, Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp alitoa wito kwa FIFA na UEFA "kutafuta suluhisho" juu ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho la Saudi Arabia mapema.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,146,3

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
FULHAM
1 | 1.28
X | 5.76
2 | 10.21

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Mwamtoro Salehe - 0652 523 XXX
2. Issaya Khimati - 0657 608 XXX
3. Erasto Mhagama - 0676 126 XXX
4. Edgar Mahund - 0678 651 XXX
5. Ruben Ruben - 0679 137 XXX
6. Stanislaus Mkuyu - 0710 179 XXX
7. Lucy Mbugano - 0711 437 XXX
8. Kedmon Chalula - 0712 432 XXX
9. Said Mdoe - 0713 107 XXX
10. Hamisi Nuru - 0716 634 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# JESUS AREJEA MAZOEZINI ARSENAL

**LONDON,** England

GABRIEL Jesus amerejea katika mazoezi ya Arsenal huku akiongeza kasi ya kupona jeraha lake la goti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alishiriki katika michezo minne ya kujiandaa na msimu kabla ya kufanyiwa upasuaji wa goti ambalo Kocha Mikel Arteta alithibitisha lilihusiana na jeraha alilopata wakati wa fainali za Kombe la Dunia.

Jesus, ambaye ana mabao 11 na asisti nane katika mechi 33 alizoichezea Arsenal, alikosa mechi 12 za Ligi Kuu England msimu uliopita kutokana na jeraha lake na bado hajacheza mwaka huu.

Arsenal watakuwa wenyeji wa Fulham leo na kuna uwezekano mkubwa Jesus hatacheza katika mchezo huo, huku Arteta akisitasita kumharakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kurejea uwanjani.

Badala yake, nafasi ya mshambuliaji wa kuanzia huenda ikachukuliwa na Eddie Nketiah, ambaye alifunga siku ya ufunguzi wa msimu na amemfunika Jesus katika kipindi chote cha majeraha yake.

Mshambuliaji mwingine, Folarin Balogun bado hajapatikana kutokana na kile kinachotajwa kuwa jeraha dogo na hakuna uhakika kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani atawahi kuichezea Arsenal tena huku klabu kadhaa Ulaya zikiwania saini yake.

Chelsea wanamtaka Balogun lakini wanasita kutoa ada inayotakiwa na Arsenal ya pauni milioni 50.

# Pochettino kuongeza wawili Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA Mauricio Pochettino amethibitisha Chelsea inataka angalau wachezaji wawili wa kusajiliwa kabla ya dirisha la usajili kufungwa kutokana na nyota majeruhi waliopo.

The Blues tayari wametumia zaidi ya pauni milioni 320 msimu huu wa joto, lakini Pochettino anataka kuongezwa fedha zaidi huku orodha ya majeruhi ikiongezeka na wachezaji tisa wakikosekana.

Mykhailo Mudryk ndiye aliyekosekana hivi karibuni baada ya kupata tatizo dogo mazoezini wiki hii huku Carney Chukwuemeka akifanyiwa upasuaji wa goti Jumatatu na anatarajiwa kuwa nje kwa takriban wiki sita.



Mchezaji mpya, Romeo Lavia hajaumia lakini hatacheza kwa mara ya kwanza "kwa wiki chache" akijaribu kupata utimamu na hiyo imechochea nia ya kuimarisha kikosi kabla ya Septemba Mosi.

Mmoja wa wachezaji wapya watakaowasili atakuwa ni kipa wa New England Revolution, Djordje Petrovic, ambaye anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kununuliwa kwa pauni milioni 14 huku Chelsea pia ikifikiria kumnunua Brennan Johnson wa Nottingham Forest na Mmarekani anayeichezea Arsenal, Folarin Balogun.

"Tunahitaji angalau kipa mmoja," alisema Pochettino Alhamisi. "Tuna walinzi chipukizi wenye vipaji, lakini wanahitaji muda. Tunahitaji zaidi na kisha tukazungumza kuhusu mchezaji mmoja mkabaji.

"Kama tunaweza kuongeza wasifu sahihi, ndio, lakini sio kuleta wachezaji ili tuongeze mwingine.

Wengi wao ni bahati mbaya," alisema Pochettino. "Nkunku na Carney au Fofana. Unawezaje kudhibiti? Sio juu ya mafunzo au mafunzo kwa bidii au kidogo au sana au mbinu. Wakati mwingine hutokea.

322,426/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/08/23 | 17:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.26 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/08/23 | 20:00 | Cadiz CF vs UD Almeria | 2.23 | 3.25 | 3.05 |
| 03. 26/08/23 | 20:00 | SC Farense vs GD Chaves | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 04. 26/08/23 | 20:30 | Granada CF vs RCD Mallorca | 2.55 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 26/08/23 | 21:45 | KV Kortrijk vs Standard Liege | 2.95 | 3.45 | 2.21 |
| 06. 26/08/23 | 22:00 | Excelsior Rotterdam vs Fortuna Sittard | 2.22 | 3.50 | 2.90 |
| 07. 27/08/23 | 02:30 | New York Red Bulls vs Inter Miami CF | 2.40 | 3.30 | 2.50 |
| 08. 27/08/23 | 13:15 | PEC Zwolle vs FC Utrecht | 2.90 | 3.60 | 2.21 |
| 09. 27/08/23 | 16:00 | Strasbourg Alsace vs Toulouse FC | 2.09 | 3.50 | 3.20 |
| 10. 27/08/23 | 16:30 | FSV Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.48 | 3.45 | 2.55 |
| 11. 27/08/23 | 17:00 | St. Truidense VV vs Cercle Brugge | 3.05 | 3.30 | 2.23 |
| 12. 27/08/23 | 17:00 | St Mirren FC vs Aberdeen FC | 2.41 | 3.20 | 2.85 |
| 13. 27/08/23 | 17:30 | Boavista Porto vs Casa Pia Lisbon | 2.22 | 3.15 | 3.20 |
| 14. 27/08/23 | 17:45 | SC Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.26 | 3.50 | 2.85 |
| 15. 27/08/23 | 18:00 | Racing Club de Ferrol vs Sporting Gijon | 2.31 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 27/08/23 | 18:00 | Sandefjord Fotball vs FK Haugesund | 2.21 | 3.20 | 2.80 |
| 17. 27/08/23 | 18:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.11 | 3.75 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 26/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3220 | Ross County vs Rangers | 7.75 | 5.17 | 1.31 |
| 14:30 | 5781 | Bournemouth vs Tottenham | 3.56 | 3.87 | 1.96 |
| 15:00 | 2998 | Bandari vs Tusker | 2.81 | 2.91 | 2.50 |
| 15:00 | 3587 | Ingolstadt vs Saarbrucken | 2.63 | 3.46 | 2.44 |
| 15:00 | 4521 | Zenit St Petersburg vs Ural Yekaterinburg | 1.50 | 4.01 | 5.75 |
| 15:00 | 4684 | Gor Mahia vs Sofapaka | 1.58 | 3.40 | 5.80 |
| 15:00 | 5374 | Kariobangi Sharks vs Kenya Police | 3.25 | 2.85 | 2.27 |
| 15:00 | 5467 | Nzoia United vs Ulinzi Stars | 2.19 | 2.90 | 3.35 |
| 16:00 | 1935 | Zanaco vs Forest Rangers | 2.21 | 2.60 | 3.50 |
| 16:00 | 4672 | Bordeaux vs Amiens | 1.66 | 3.71 | 4.55 |
| 16:30 | 1695 | FC Koln vs VfL Wolfsburg | 2.34 | 3.55 | 2.93 |
| 16:30 | 2839 | VfL Bochum vs Borussia Dortmund | 6.38 | 5.15 | 1.43 |
| 16:30 | 3266 | SC Freiburg vs Werder Bremen | 1.72 | 3.96 | 4.63 |
| 16:30 | 3588 | Heidenheim vs Hoffenheim | 2.99 | 3.61 | 2.28 |
| 16:30 | 4565 | SV Darmstadt vs Union Berlin | 3.96 | 3.50 | 1.95 |
| 17:00 | 1651 | Preston vs Swansea | 2.48 | 3.18 | 2.68 |
| 17:00 | 1840 | Huddersfield vs Norwich City | 3.21 | 3.36 | 2.08 |
| 17:00 | 2184 | Southampton vs QPR | 1.34 | 4.76 | 7.54 |
| 17:00 | 2596 | Cardiff vs Sheffield Wed | 2.12 | 3.17 | 3.31 |
| 17:00 | 2672 | Celtic vs St Johnstone | 1.04 | 10.93 | 28.81 |
| 17:00 | 3692 | Peterborough vs Derby | 2.44 | 3.35 | 2.70 |
| 17:00 | 3962 | Millwall vs Stoke City | 2.30 | 3.13 | 2.98 |
| 17:00 | 4388 | Manchester Utd vs Nottingham | 1.38 | 5.14 | 7.80 |
| 17:00 | 4421 | Everton vs Wolverhampton | 2.34 | 3.29 | 3.13 |
| 17:00 | 4886 | Birmingham vs Plymouth | 1.84 | 3.33 | 4.07 |
| 17:00 | 5117 | Brentford vs Crystal Palace | 2.09 | 3.40 | 3.60 |
| 17:00 | 5137 | Motherwell vs Kilmarnock | 2.33 | 3.18 | 2.93 |
| 17:00 | 5161 | Coventry vs Sunderland | 2.07 | 3.32 | 3.27 |
| 17:00 | 5344 | Wigan vs Barnsley | 2.18 | 3.46 | 3.01 |
| 17:00 | 5738 | Rotherham vs Leicester | 5.14 | 3.86 | 1.57 |
| 17:00 | 5819 | Ipswich vs Leeds | 2.25 | 3.22 | 2.98 |
| 17:00 | 5872 | Arsenal vs Fulham | 1.28 | 5.76 | 10.21 |
| 17:00 | 5971 | West Bromwich vs Middlesbrough | 2.16 | 3.37 | 3.02 |
| 17:30 | 5466 | Rubin Kazan vs Dinamo Moscow | 2.93 | 3.39 | 2.20 |
| 18:30 | 1554 | Kaizer Chiefs vs Amazulu | 2.02 | 2.93 | 3.96 |
| 19:30 | 1152 | Frosinone vs Atalanta | 4.73 | 3.96 | 1.71 |
| 19:30 | 2044 | Brighton vs West Ham | 1.55 | 4.61 | 5.33 |
| 19:30 | 4512 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 3.61 | 4.02 | 1.91 |
| 19:30 | 4598 | Monza vs Empoli | 1.95 | 3.50 | 3.96 |
| 20:00 | 1392 | Cadiz CF vs Almeria | 2.26 | 3.34 | 3.24 |
| 20:00 | 3479 | Marseille vs Brest | 1.54 | 4.43 | 5.77 |
| 20:30 | 3876 | Granada vs Mallorca | 2.63 | 3.04 | 2.94 |
| 21:00 | 3389 | Stellenbosch vs SuperSport Utd | 3.14 | 2.88 | 2.36 |
| 21:30 | 4802 | Hannover vs Hamburger SV | 3.10 | 3.85 | 2.01 |
| 21:45 | 2917 | Kortrijk vs Standard Liege | 2.94 | 3.44 | 2.20 |
| 21:45 | 5218 | AC Milan vs Torino | 1.71 | 3.63 | 5.30 |
| 21:45 | 5244 | Verona vs Roma | 4.42 | 3.45 | 1.87 |
| 22:00 | 2218 | Paris St Germain vs Lens | 1.66 | 4.00 | 5.07 |
| 22:30 | 2707 | Sevilla FC vs Girona | 2.13 | 3.45 | 3.45 |
| 22:30 | 4605 | Gil Vicente vs Benfica | 8.36 | 5.37 | 1.28 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# JKT QUEENS KAMILI KUIVAA BUJA NUSU FAINALI CECAFA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha JKT Queens kinatarajia kukutana na Buja Queens ya Burundi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA) itakayofanyika kesho nchini Uganda.

JKT Queens ambayo iliingia hatua ya nusu fainali baada ya kumaliza kinara katika Kundi B, ikikusanya pointi tisa wakati Buja ilikuwa nyuma ya vinara Vihiga Queens ya Kenya katika Kundi A. Mechi nyingine ya nusu fainali itachezwa leo kati ya Vihiga Queens dhidi ya CBE kutoka Ethiopia.

Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, amesema pambano hilo litakuwa ni moja kati ya mechi bora kwenye michuano hiyo msimu huu kutokana na ubora ya vikosi vyote, lakini anaamini watashinda na kusonga mbele.

Chabruma alisema timu yake imejipanga vizuri lakini wataingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao.

"Mimi ninaiamini timu yangu, nimeiandaa vizuri kuhakikisha tunacheza nusu fainali ambayo itakuwa bora na tunapata ushindi, najua Buja ni timu nzuri sana na wamekuja kwenye mashindano kushindana, lakini wajue pia na sisi tumekuja kushindana," alisema Chabruma.

Mabingwa wa Tanzania, JKT Queens wako kwenye harakati ya kuusaka ubingwa wa CECAFA ambao ulikuwa unashikiliwa na Simba Queens ya Tanzania pia.

Bingwa wa mashindano hayo atawakilisha CECAFA katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Ivory Coast.



Wachezaji wa Namungo FC ya Lindi wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara zitakazoendelea tena baada ya kalenda ya kimataifa kumalizika. **PICHA: MTANDAO**

## *Gamondi ataka mabao,*

INATOKA UK 24

"Mechi ya kesho (leo) tunaanza upya, nimewaambia wachezaji wangu kusahau matokeo ya mechi iliyopita na tunaanza upya kabisa, nataka kuona mchezo mzuri na ushindi wa mabao mengi.

Kila mchezaji anatakiwa kupambana kwa sababu kila mtu anayo nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza, Hafiz (Konkoni) ni mzuri na bado anahitaji muda ili kuwa mzuri zaidi," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa kila mchezaji anapaswa kuwa tayari ukiangalia safu ya kiungo Pacome Zouzoua na Stephane Aziz Ki wameonyesha kiwango kizuri na kumpaa ushawishi mkubwa.

Gamondi alisema kuwa wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo na anahitaji kupata matokeo mazuri nakukoleza safari ya kufikia malengo yao msimu huu ya angalau kufikia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo hawajawahi kufika kwenye hatua hiyo.

"Msimu uliopita timu ilifanya vizuri kweye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kufika fainali, msimu huu tumeanza mashindano mengine, Ligi ya mabingwa tuna malengo yetu kama timu, mchezo wa kesho wa marudiano ni sehemu ya safari yetu kufikia malengo tuliyojiwekea," alisema Gamondi.

Mchezo huo wa leo unachezwa kwenye uwanja wa Azam Complex baada ya uwanja wa Benjamin Mkapa kufungwa kwa muda kwa ajili ya matengenezo makubwa.

## PENALTI ZAWAONDOA AZAM

INATOKA UK 24

yalitoka juu ya lango la Azam FC.

Ilikuwa ni kama kumfukuza mwizi wakati umeacha mlango wazi, kwani baada ya mashambulizi hayo, dakika ya tisa, Azam iliandika bao la pili kupitia kwa Mzimbabwe Prince Dube.

Cheikh Sidibe aliupenyeza mpira wingi kushoto, safari hii ukamkuta Feisal Salum ambaye aliambaa ya mpira kwenye chaki, kabla ya kumimina majario yaliyomkuta mfungaji ambaye alikwamisha kwa mguu wa kulia.

Bahir Dar Kenema wapata bao laodakika ya 19 kupitia kwa Tadesse aliyepenyezewa pasi safi kutoka kwa Fitsun Tulahun ambapo kipa wa Azam Iddrisu alichelewa kutoka na mfungaji aliudokoa mpira uliompita Iddrisu katikati ya miguu yake na kujaa wavuni.

Dakika mbili baadaye Dube akosa mabao mawili ya wazi yote yakigonga mwamba, dakika ya 21 na hatari kubwa zaidi ilikuwa katika dakika ya 43 baada ya kumpiga chenga kipa Malko, lakini shuti lake hafifu liligonga nguzo ya chini na kurejea uwanjani kabla ya kuokolewa na mabeki wa Kanema.

Kipindi cha pili, Azam ilifanya mabadiliko ikiwatoa Dube, Sopu na James Alaminko, na kuwaingiza Mbombo, Bangala na Kipre Junior na dakika moja tu baada ya kuingia, Mbombo alikosa bao la wazi akiwa ndani ya eneo la hatari shuti lake likikamatwa na kipa Malko.

# Michezo

Jumamosi Agosti 26, 2023
Nipashe


UK. 21




Liverpool: Salah hawezi kuondoka

# Gamondi ataka mabao, soka safi Yanga leo




●●● Asema licha ya ushindi mchezo wa kwanza, hawakucheza vizuri lakini leo anataka kuwabana Asas FC kila idara..

**Na Saada Akida**

MWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga leo inashuka kwenye uwanja wa Azam Complex kucheza mchezo wa marudiano hatua ya awali dhidi ya AS Al Sabieh (Asas FC) kutoka Djibouti huku kocha Miguel Gamondi akitaka kikosi chake licha ya kusaka mabao ya kutosha pia kicheze soka safi la kuwafurahisha mashabiki wao.

**Gamondi alisema kwenye mchezo wa kwanza licha ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0, hawakucheza vizuri na hataki jambo hilo lijirudie leo na tayari amefanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mchezo wa kwanza.**

"Ni mchezo muhimu sana, natarajia mabadiliko makubwa ya kiuchezaji, tunataka ushindi lakini pia tucheze soka safi kwa ajili ya mashabiki wetu, tunapaswa kutumia kila nafasi tunayoipata na naamini tutafanikiwa malengo yetu kwenye mchezo huu," alisema Gamondi.

Yanga wanahitaji kushinda kwenye mchezo wa leo ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo na kama atafanikiwa atakutana na mshindi wa mchezo kati ya El Marreikh ya Sudan na Otoho FC ya Congo Brazzavile.

Gamondi alisema anafahamu sare au ushindi wowote utawavusha kuelekea hatua inayofuata lakini amewaambia wachezaji wake watumie vyema nafasi watakazozipata ili kupata ushindi mzuri utakaowapa hamasa kuelekea kwenye mchezo unaofuata wa michuano hiyo.

INAENDELEA UK 23

# PENALTI ZAWAONDOA AZAM SHIRIKISHO CAF



**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena Azam FC imeshindwa kusonga mbele kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho baada ya kung'olewa katika hatua ya awali dhidi ya Bahir Dar Kenema ya Ethiopia kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Msimu uliopita Azam iliondolewa raundi ya kwanza ya michuano hiyo kwa jumla ya mabao 3-2 dhidi ya Al Akhdar ya Algeria, ikifungwa mabao 3-0 ugenini na kushinda nyumbani mabao 2-0.

Timu hizo jana zililazimika kupigiana penalti baada ya Azam kumaliza dakika 90 kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1, ambao ulifanana na matokeo ya Jumapili iliyopita, Bahir Dar Kenema ikishinda kwa idadi hiyo ya mabao kwenye uwanja wake wa nyumbani Abebe Bikila, hivyo kulazimika kupigiana mikwaju ya penalti baada ya matokeo ya jumla kuwa 3-3.

Kipa wa Azam FC, Addullau Iddrisu aliokoa mikwaju miwili ya penalti, lakini haikusaidia kwani Jibril Sillah alikosa baada ya kugongesha nguzo, Sospeter Bajana alipaisha na penalti ya Idris Mbombo ikiokolewa na kipa Alazar Markos Malko.

Wachezaji wa Azam waliofunga penalti zao ni Yannick Bangala, Feisal Salum na Cheikh Sidibe.

Waliotupia upande wa Dar Bahir Kenema ni Yared Bayeh, Fikremikael Alemu, Salamlak Tegegn na Alelign Azene, huku waliokosa kwa kupanguliwa na kipa Iddrisu ni Fitsum Tilahun na Yabsira Tesfaye.

Kabla ya hapo Azam ilianza biashara asubuhi dakika ya kwanza tu, Idd Suleiman 'Nado' alipapachika bao la kwanza alipobaki yeye na nyavu na kufunga kirahisi.

Aliuanzisha mwenyewe shambulizi katikati ya uwanja kwa kuupiga mpira winga ya kushoto kwa Prince Dube ambaye alipiga krosi ndefu iliyovuka lango, ukamkuta Yahya Zaid ambaye alirudisha golini na kumkuta Nado akiwa ameshaingia kwenye eneo la hatari, akakutana nao ana kwa ana kabla ya kuukwamisha wavuni.

Bao hilo lilionekana kama kuwachefua Bahir Dar Kanema kwani walianza msako kwa mashambulizi mfululizo dakika ya tano na ya sita kwa mashuti makali

INAENDELEA UK 23

## Mzamiru, Ngoma wampasua kichwa kocha Robertinho

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amekiri kuwa anapata wakati mgumu kuamua nani wa kuanza kati ya viungo wake wawili, Mzamiru Yassin na Frabrice Ngoma kutokana na ubora wa wachezaji hao.

Robertinho alisema Mzamiru na Ngoma wana uwezo mkubwa na kwa sasa wapo kwenye viwango vya juu na wamekuwa msaada mkubwa kwenye kikosi cha timu hiyo.

Robertinho ametoa kauli hiyo kutokana na ubora wa viungo hao katika eneo la kati kwa kuweza kuituliza timu na kuweza kutengeneza mashambulizi ambapo mpaka sasa Simba imefanikiwa kushinda mechi nne za mashindano zikiwemo mbili za Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema ubora mkubwa unaonyeshwa na safu yake ya kiungo cha kati kinapelekea kutokuwa na mchezaji mwenye nafasi ya uhakika kutokana na wote kuwa kwenye ubora unaofanana katika kutekeleza majukumu ya timu ndani ya uwanja.

Alisema kila mchezaji amekuwa akionyesha kiwango kizuri kwa kutengeneza muunganiko mkubwa hali iliyopeleka kufanya vizuri na kutengeneza mashambulizi mengi.

"Timu ipo kwenye wakati mzuri kwa ajili ya mashindano ambayo yapo mbele yetu kutokana ukubwa wake, ukiangalia tuna ligi ya mabingwa, Super league, Kombe FA pamoja na michuano ya mapinduzi lakini napata furaha zaidi kwa sababu karibu kila idara wachezaji wamekuwa wakionyesha ubora wa kiwango kikubwa ambacho kinachangia kupata matokeo mazuri.



"Hakuna ambaye anaweza kusema kuwa na nafasi ya kudumu ndani ya timu yangu kwa sababu wote wamekuwa katika ubora mkubwa, angalia eneo la kati kuna Mzamiru, Ngoma pamoja na Kanuti ambao wote wanaisadia timu kwa kutimiza majukumu yao kwa kila ambaye anapata nafasi ya kucheza," alisema Robertinho.

Alisema anawapongeza viongozi wa timu hiyo kwa kufanya usajili mzuri kwa wachezaji ambao wote wana uwiana kiuwezo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >